United Nations
TANZANIA
Delivering as One

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA MAKAMU WA RAIS

# MWONGOZO WA KUFUNDISHIA UHUSIANO KATI YA UMASKINI NA MAZINGIRA

## MWONGOZO WA MWEZESHAJI

IDARA YA MAZINGIRA

2011

# MWONGOZO WA KUFUNDISHIA UHUSIANO KATI YA UMASKINI NA MAZINGIRA

## MWONGOZO WA MWEZESHAJI

# YALIYOMO

**ORODHA YA MAJEDWALI** ..... **iv**
**ORODHA YA MICHORO** ..... **v**
**ORODHA YA VISANDUKU** ..... **v**
**VIFUPISHO** ..... **vi**
**DIBAJI** ..... **vii**
**SHUKRANI** ..... **viii**

**UTANGULIZI** ..... **ix**
Madhumuni ya Kitini ..... ix
Ufundishaji ..... x
Mbinu za Ufundishaji ..... x
Matokeo yanayotarajiwa ..... xi
Walengwa Wanaokusudiwa ..... xi
Marejeo ..... xii

**MODULI YA KWANZA** ..... **1**
Uhusiano wa Umaskini na Mazingira ..... 1
Maswali ya mjadala ..... 15

**MODULI YA PILI:** ..... **17**
Utawala na Mchakato wa Sera za Nchi ..... 17

**MODULI YA TATU:** ..... **36**
Nadharia ya mfumo-ikolojia katika Uhusiano wa Umaskini na Mazingira ..... 36

**MODULI YA NNE** ..... **46**
Kugharamia Uhifadhi wa Mazingira ..... 46
Nafasi ya Msaada wa Ujumla kupitia bajeti kwa sekta ya mazingira .. 54

# ORODHA YA MAJEDWALI


| Namba ya Jedwali | Maelezo ya Jedwali | Ukurasa |
|---|---|---|
| 1.1 | Maeneo muhimu ya kuyafanyia kazi kisera | 14 |
| 2.1 | Hatua katika Harakati za kulinda Mazingira | 20 |
| 2.2 | Uainishaji wa mbinu za kisera kuhusu Mazingira | 23 |
| 2.3 | Muhtasari wa malengo mahsusi kuhusu Mazingira katika MKUKUTA | 29 |
| 2.4 | Mifano ya mikakati ya utekelezaji wa Malengo yanayohusiana na mazingira yaliyopo katika MKUKUTA | 30 |
| 2.5 | Mazingira na Malengo ya Maendeleo ya Milenia | 34 |
| 3.1 | Mambo yanayoashiria ustawi wa jamii yenye matatizo kimikoa | 42 |


# ORODHA YA MICHORO


| Namba ya Mchoro | Maelezo ya Mchoro | Ukurasa |
|---|---|---|
| 3.1 | Hatua za kutathmini mifumo ya ikilojia | 44 |

# ORODHA YA VISANDUKU


| Namba ya Kisanduku | Maelezo ya Kisanduku | Ukurasa |
|---|---|---|
| 1.1 | Maskini ni nani? | 2 |
| 1.2 | Mifano ya uhusiano wa idadi ya watu, umaskini na mazingira | 4 |
| 1.3 | Mfano: Kuhifadhi njia za kujipatia riziki na mazingira nchini Tanzania | 8 |
| 1.4 | Mifano ya usimamizi mbovu wa mazingira na athari zake katika ukuaji wa uchumi | 9 |
| 1.5 | Maeneo ya hifadhi na watu maskini: utata katika shughuli za uhifadhi? | 11 |
| 1.6 | Kunufaika kutokana na maeneo ya hifadhi | 12 |
| 2.1 | Mfano wa Uzingatifu wa utawala wa kimazingira nchini Tanzania | 18 |
| 3.1 | Njia endelevu za kujipatia riziki | 38 |
| 3.2 | Viukilio muhimu vya ustawi | 39 |
| 4.1 | Baadhi ya mambo ya msingi juu ya mifuko ya mazingira | 48 |
| 4.2 | Kanuni ya Mchafuzi Kugharamia | 49 |
| 4.3 | Changamoto za Utekelezaji wa Kanuni | 49 |
| 4.4 | Vigezo vya Mifuko ya Mazingira | 51 |
| 4.5 | Changamoto za Mikakati ya Kupunguza Umaskini | 55 |
| 4.6 | Mfano wa tatizo la utawala mbovu katika usimamizi wa maliasili | 58 |
| 4.7 | Kiwango cha Matumizi ya Fedha za Umma | 59 |
| 4.8 | Tafsiri ya Matumizi ya Fedha za Umma | 60 |

# VIFUPISHO

| | | |
|---|---|---|
| UKIMWI | - | Upungufu wa Kinga Mwilini |
| AZAKI | - | Asasi za Kijamii |
| CPP | - | Mpango wa Kushindanisha Miradi |
| AZAKI | - | Asasi za Kijamii |
| DPs | - | Washirika wa maendeleo |
| EIA | - | Tathmini ya Athari kwa Mazingira |
| GBS | - | Msaada wa Jumla katika Bajeti |
| GDP | - | Pato la Taifa |
| VVU | - | Virusi Vya Ukimwi |
| FBO | - | Mashirika ya Kidini |
| HBS | - | Utafiti wa Bajeti za Kaya |
| LGA | - | Mamlaka ya Serikali za Mitaa |
| MDAs | - | Wizara, Idara na Mashirika ya Serikali |
| M&E | - | Uperembaji na Tathmini |
| MDG | - | Malengo ya Maendeleo ya Millenia |
| MKUKUTA | - | Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kuondoa Umaskini |
| MOFEA | - | Wizara ya Fedha na Uchumi |
| NEMC | - | Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira |
| AZISE | - | Asasi Zisizo za Serikali |
| NR | - | Maliasili |
| NSGRP | - | MKAKATI wa Taifa wa Kukuza Uchumi na Kuondoa Umaskini |
| PA | - | Maeneo ya Hifadhi |
| PER | - | Mapitio ya Matumizi ya Umma katika sekta ya Mazingira |
| PES | - | Kugharamia Huduma zitokanazo na mazingira |
| PRS | - | Mkakati wa Kupunguza Umaskini |
| SSA | - | Afrika ya Kusini mwa Jangwa la Sahara |
| SWG | - | Makundi ya Harakati za Kimazingira |
| UNDP | - | Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa |
| WHO | - | Shirika la Afya Duniani |

# DIBAJI

Kuhuisha shughuli za hifadhi ya mazingira katika mipango ya maendeleo ni jambo la kuzingatia ili kuwa na maendeleo endelevu katika Taifa. Hapo awali, mijadala na juhudi za maendeleo zililenga zaidi katika kukuza uchumi bila kuzingatia athari za shughuli za maendeleo katika mazingira. Mwenendo huu ulisababisha maendeleo yasiyo endelevu.

Kitini hiki cha mafunzo kuhusu Uhusiano kati ya Umaskini na Mazingira kimetayarishwa kwa ajili ya kukuza uelewa wa watendaji katika ngazi mbalimbali ili waweze kupanga na kutekeleza mipango inayozingatia hifadhi ya mazingira. Juhudi za kukuza uchumi na kuondoa umasikini hazina budi kuweka bayana jinsi matumizi endelevu ya rasilimali yatakavyoanishwa katika sera, programu, mikakati, sheria na mipango ya maendeleo.

Dira ya Taifa ya Maendeleo kuelekea mwaka 2025 na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kuondoa Umaskini (MKUKUTA) ni juhudi za Serikali katika kuratibu mipango na juhudi za maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa kuzingatia hifadhi ya mazingira kama eneo mtambuka ambalo hapo awali halikuwa linazingatiwa katika mipango na mikakati ya kuondoa umaskini nchini. Kuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya uharibifu wa mazingira na umaskini. Uharibifu wa mazingira huchangia kuongezeka kwa umaskini, vivyo hivyo, umaskini mara nyingi huchangia katika uharibifu wa mazingira kwa kuwa hukwamisha juhudi za jamii katika kusimamia matumizi endelevu ya rasilimali zao.

Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali imeandaa kitini hiki kwa ajili ya kufundisha watendaji hasa katika mamlaka za Serikali za Mitaa, idara za serikali, mashirika yasiyokuwa ya kiserikali na wadau mbalimbali wanaohusika katika utayarishaji wa mipango na programu mbalimbali za maendeleo katika maeneo yao.

Ni imani yangu kuwa kitini hiki kitatumika ipasavyo ili kukuza uelewa kuhusu uhusiano kati ya umaskini na mazingira na kuchangia juhudi za kuleta maendeleo endelevu.

**Dkt. Therezya Luoga Huvisa, (MB)**
**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira**
**Machi, 2011**

# SHUKRANI

Kukamilika kwa maandalizi ya Kitini hiki kinachoainisha uhusiano kati ya umaskini na mazingira ni matokeo ya juhudi za taasisi na wataalam mbalimbali waliotumia muda na utaalam wao katika kazi hii. Pamoja na kuwa ni vigumu kumtaja kila mmoja na mchango wake, napenda kuchukua fursa hii ya pekee kutambua mchango wa taasisi na baadhi ya wataalam.

Napenda kutoa shukrani kwa Ofisi ya Waziri Mkuu-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; na Wizara ya Fedha na Mipango. Vilevile, natambua ushiriki wa taasisi zifuatazo: Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam–Idara ya Uchumi kwa michango yao ya kiufundi iliyowezesha kukamilika kwa kitini hiki.

Aidha, nalishukuru Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) Tanzania kwa kugharamia zoezi hili kupitia Mradi wa Kuhuisha masuala ya mazingira katika utekelezaji wa MKUKUTA unaoratibiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais (OMR).

Shukurani za pekee nazitoa kwa timu ya wataalamu wa Ofisi ya Makamu wa Rais walioshiriki katika kusimamia maandalizi ya kitini hiki.

**Sazi Salula**
**Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais**
**Machi, 2011**

# UTANGULIZI

**Madhumuni ya Kitini**

Tatizo la msingi katika maisha ya binadamu ni jinsi ya kukidhi mahitaji mengi na yasiyokoma katika vyanzo vichache. Mkabala wa wanauchumi kwa tatizo hili ni kuhakikisha kwamba mahitaji haya yanatimizwa katika njia sahihi (bila kuathiri mtu yeyote) na yenye ufanisi (rasilimali zinatumika katika njia bora ili kuzalisha kiasi cha kutosha). Kuhusisha masuala ya uhifadhi wa mazingira katika mkabala wa wanauchumi kunaleta dhana ya uendelevu: ni kwa jinsi gani mahitaji ya binadamu wa leo yanaweza kutimizwa katika njia ambazo hazitaathiri uwezo wa kutimiza mahitaji kama hayo ya vizazi vijavyo.

Mtazamo wa jumla wa kitini hiki cha kufundishia ni juu ya uhusiano baina ya umaskini na mazingira.Lengo ni kuonesha ni kwa jinsi gani mabadiliko ya ubora wa mazingira yanawaathiri watu wanaoyategemea. Vigezo vikuu vya umaskini ambavyo vinazingatiwa ni njia za kujipatia kipato, afya bora na utawala bora. Kitini hiki kina moduli nne ambazo ni:-

a) Maelezo ya Jumla ya Uhusiano wa Umaskini na Mazingira
b) Utawala na usimamizi wa mazingira asilia
c) Nadharia ya mfumo wa ikolojia katika uhusiano wa umaskini na mazingira
d) Ugharamiaji wa usimamizi wa mazingira

Kitini kimeandaliwa ili kitumiwe na watunga sera na wadau wa masuala ya uhifadhi wa mazingira na kuondoa umaskini. Moduli zimekusudiwa kufundishwa katika warsha au maeneo mengine ya mafunzo kwa njia ambazo ni shirikishi, ili wawezeshaji na washiriki washirikiane katika, mawasilisho, mihadhara na mijadala, kama nyongeza ya kazi za vikundi na mawasilisho ya mifano mahsusi.

Madhumuni ya kuandaa kitini hiki ni kuwezesha harakati halisi za mwamko wa masuala ya mazingira na umaskini katika sera, mipango na

michakato ya usimamizi wa Mazingira nchini, kwa kuonesha uhusiano uliopo baina ya umaskini na mazingira kwa upande mmoja na ukuaji wa uchumi kwa upande mwingine.

Zaidi ya kuonesha mambo muhimu ya kidhana ya uhusiano wa umaskini na mazingira, kitini hiki:

a) Kinatoa marejeo ya dhana, mikakati, sera na miongozo;
b) Kinajadili masuala ya kimkakati yanayohusiana na mipango, utekelezaji na tathmini ya sera na mikakati ya mazingira ;
c) Kinabainisha wahusika wakuu wa shughuli za uhifadhi na wadau wengine.

Kitini kinakusudia:

a. Kutoa ujuzi unaohitajika kwa watunga sera na wadau wengine ili kuchanganua uhusiano wa umaskini na mazingira;
b. Kuwatambulisha wadau kwa mbinu mbalimbali zinazotumika katika kuchanganua uhusiano wa umaskini na mazingira
c. Kubainisha kazi na majukumu ya wahusika mbalimbali na wadau wa uhifadhi wa mazingira katika kuendeleza michakato ya kisera inayohusu uhusiano kati ya umaskini na mazingira;
d. Kusaidia katika kuelezea viashiria vya uhusiano wa umaskini na mazingira kwa ajili ya usimamizi wa sera na mikakati,
e. Kubainisha mbinu mbalimbali ya kupata vyanzo vya fedha kwa ajili ya shughuli za usimamizi wa mazingira.

**Ufundishaji**

Kila kipindi cha moduli kipewe muda wa kutosha ili kuwezesha ushirikiano baina ya wawezeshaji na washiriki wa mafunzo, yakiwemo kazi-mazoezi ya vikundi na mawasilisho.

**Mbinu za Ufundishaji**

Inashauriwa kwamba wakufunzi watumie mbinu mbalimbali zilizozoeleka katika kufundisha na kuongoza vipindi husika. Miongoni mwa mbinu hizo ni:

a) Mawasilisho;

b) Mihadhara;
c) Kazi za vikundi vidogo vidogo;
d) Mijadala katika vikundi vikubwa; na
e) Mapitio ya mifano mahsusi inayohusiana na kipindi husika.

Ni muhimu kwa wakufunzi wote kuhakikisha wanaongoza kila kipindi katika namna ambayo kutakuwa na mtiririko wa kimantiki. Hili linaweza kufanywa kwa kuchagua na kutumia mikabala iliyozoeleka na inayokubalika katika ufundishaji, kama vile kuonesha na kubainisha kazi mahsusi kwa kila moduli/kipindi. Baadhi ya maswali ya mwongozo yanayoweza kutumiwa na wawezeshaji katika kufanikisha somo husika yanapatikana mwishoni mwa kila moduli. Wawezeshaji wanahimizwa kutumia maswali mengine yanayofaa.

**Matokeo yanayotarajiwa**

Mwisho wa mafunzo, washiriki wanatarajiwa:

a) Kuelewa na kuthamini dhana na umuhimu wa kuhusisha umaskini na mazingira katika michakato ya kutoa maamuzi ;
b) Kuelewa mchango wa mazingira katika kukuza uchumi wa taifa;
c) Kuelewa mchakato wa kubuni, kutekeleza na kutathmini viashiria vya umaskini na mazingira;
d) Kutumia mbinu, njia mahsusi na mifano halisi katika jamii zinazopaswa kuzingatiwa ili kuelezea mahusiano ya umaskini na mazingira;
e) Kuelewa juhudi na mikakati ya kitaifa na kimataifa katika uhifadhi wa mazingira;
f) Kuwa mahiri katika kueleza uhusiano baina ya utawala, uhifadhi wa maliasili na njia kuu za kujipatia riziki; na
g) Kuelewa mikabala mbalimbali na utaratibu unaoweza kutumika kugharamia uhifadhi wa mazingira.

**Walengwa Wanaokusudiwa**

Kiuhalisia, uelewa wa uhusiano wa umaskini na mazingira unamhusu karibu kila mtu, hata hivyo kitini hiki kinawalenga zaidi watunga sera, watoa maamuzi na watekelezaji wa sera na programu zinazoathiri

mazingira. Washiriki waliokusudiwa wanajumuisha wafuatao:-

a) Watunga sera au mawakala wa sera ;
b) Maafisa wa serikali (serikali kuu na serikali za mitaa) wanaohusika na utekelezaji wa sera;
c) Waandaaji wa programu za maendeleo au mameneja;
d) Waajiri;
e) Mashirika ya kijamii (CBOs);
f) Asasi za kijamii (AZAKI); na
g) Mashirika ya dini (FOBs).

**Marejeo**

Bojo, J, K-G Maler and L. Unenmo. 1992. *Environment and Development: An Economic Approach.* Kluwer Academic Publishers

*Environment and Development Economics*, Cambridge University Press

Kiss, A and D. Shelton. 1992. Manual of European Environmental Law, Grotius Publications, Cambridge

United Nations. 1992. *Earth Summit Agenda 21: The United Nations Programme of Action From Rio*, United Nations, New York

# MODULI YA KWANZA

## Uhusiano wa Umaskini na Mazingira

### Malengo ya Moduli

**Kipindi cha Kwanza**
Moduli hii inakusudia kuwapa watunga sera na wadau, maelezo ya jumla ya uhusiano wa msingi baina ya umaskini na mazingira katika maeneo ya vijijini na mijini, pamoja na tafsiri ya kisera katika ngazi za chini, za kati na za juu. Katika moduli hii tunaangalia uhusiano wa umaskini na mazingira kwa kutathmini jinsi mazingira na mabadiliko ya kimazingira katika maeneo ya vijijini na mijini yanavyoathiri watu maskini, katika maeneo makuu matatu ya umaskini ambayo ni njia za kujipatia kipato, afya bora na utawala bora. Lengo ni kuwapa washiriki uelewa wa baadhi ya dhana za msingi za uhusiano huu.

**Muda uliopendekezwa**
Muda usiozidi saa tatu utatumika kuwasilisha mada zilizoko katika moduli hii ikijumuisha angalau dakika 30 za utangulizi unaoelezea hali halisi ya mazingira na umaskini nchini Tanzania._

**Mbinu za ufundishaji**
Katika kipindi hiki inashauriwa kutumia mchanganyiko wa mbinu, zikiwemo mawasilisho mafupi, kazi za vikundi na mapitio ya mifano mahsusi na nyaraka zifaazo pamoja na taarifa za nyongeza kuhusu maelezo ya jumla ya umaskini na mazingira katika Tanzania.

**Kazi za kufanya**

**Maelezo ya jumla ya umaskini na mazingira**
Kujadili hali ya umaskini na mazingira nchini Tanzania kwa kipindi cha miaka 40 au zaidi iliyopita. Waeleze washiriki hatua na mambo

mbalimbali yaliyofanywa tangu suala hili kuwa la kimataifa. Onyesha hatua mbalimbali na mikakati iliyochukuliwa na serikali na wadau katika kushughulikia matatizo haya.

- Kumbuka kutaja na kujadili baadhi ya mambo muhimu yafuatayo:-

**Kisanduku Na. 1.1: Maskini ni nani?**

Hadi miaka ya 1970, umaskini kwa kawaida ulitafsiriwa kuwa ni kushuka kwa upatikanaji wa chakula, kipato au matumizi chini ya kiwango fulani. Kwa mfano Benki ya Dunia imekuwa ikitumia kiwango cha Dola moja ya Marekani kwa siku. Kwa sasa mtazamo huu finyu haukubaliki sana miongoni mwa wanasayansi jamii mashirika ya maendeleo na wadau. Katika miaka ya hivi karibuni mtazamo wa jinsi ambavyo watu maskini wanavyouona umaskini na jinsi umaskini unavyotafsiriwa katika tamaduni tofauti umepewa umuhimu mkubwa. Kwa sasa, maskini anatafsiriwa kama mtu ambaye hawezi kujitimizia mahitaji yake muhimu, kama yanavyoeleweka katika jamii husika. Hii inajumuisha ukosefu wa mahitaji muhimu ya binadamu ikilinganishwa na rasilimali, ukosefu wa usalama na uwezo wa kutoa maamuzi katika masuala yanayomhusu. Kutokana na mtazamo wa sasa wa Benki ya Dunia, " umaskini ni suala la mawanda mapana, linalojumuisha kukosekana kwa huduma bora za afya, elimu, pamoja nyanja nyingine dhahania za maisha kama vile kukosekana kwa usawa wa kijinsia, usalama, kukosekana kwa uwezo wa kufanya maamuzi na kutengwa kijamii". Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa, linatafsiri maendeleo kuwa ni "mchakato wa kuongeza fursa za binadamu kujipatia kipato". Kwa, muktadha huu, umaskini ni "kukosekana kwa fursa na nafasi za msingi kabisa kwa maendeleo ya binadamu – yanayohusiana na afya, maisha ya ubunifu na kufurahia kiwango bora cha maisha, uhuru, utu, kuheshimiwa na kuheshimu wengine.

1.1.1

Kwa kuzingatia mawanda haya mapana ya umaskini, kipimo halisi cha maskini ni nani hakiwezi kuishia kwenye kipimo cha umaskini wa kipato, bali pia kizingatie makundi ya kijamii kama vile jinsia,

makabila, mazingira waishio, hali ya njia za kujipatia riziki n.k. Tofauti pia yaweza kuwekwa kati ya watu walio katika umaskini sugu (umaskini wa muda mrefu) na wale ambao wapo katika umaskini wa mpito. Umaskini wa mpito unaweza kutokana na matatizo ya asili au ya kiuchumi. Kaya zilizo katika umaskini sugu zinaweza pia kuwekwa katika makundi, kutegemeana na tabia zao mahsusi na sababu zisizo rasmi. Kundi mojawapo la umaskini sugu laweza kuwa maskini katika nyanja kadhaa; kwa mfano, makundi yaliyotengwa kijamii, watu wenye ulemavu, wakimbizi na watu waliolazimika kuhama makazi yao, wagonjwa wa UKIMWI n.k. Kundi jingine ni la wale walio katika umaskini sugu uliosababishwa na kukosa uwezo wa kupata vyanzo vya uzalishaji mali.

| **Viashiria vya umaskini: Tanzania Bara** | **1990** | **2000/ 2001** | **2007** |
|---|---|---|---|
| | **Asilimia** | | |
| Wastani wa idadi ya watu waishio chini ya kiwango cha Umaskini wa kupata mahitaji yao muhimu | 39 | 36 | 33.2 |
| Wastani wa idadi ya watu wanaoishi chini ya kiwango cha umaskini wa kupata chakula | 22 | 19 | 16.5 |

**Uhusiano wa umaskini na mazingira umefupishwa katika sentensi maarufu isemayo: *"Umaskini ni sababu na matokeo ya uharibifu wa mazingira."***

Mwezeshaji ajadili uhusiano wa umaskini na mazingira katika mtazamo unaojumuisha yafuatayo:

a) Umaskini unabadilika kwa kutegemea maeneo ya kijiografia, kiwango na tabia za kiuchumi, kijamii na kiutamaduni za mtu mmoja mmoja, kaya na makundi ya kijamii;

b) Kwamba uhifadhi wa mazingira unahitaji kuchambua kwa undani na kuwa na uelewa mpana wa uhusiano wa umaskini na mazingira;

c) Zaidi ya yote onesha kwamba uhifadhi wa mazingira unajibainisha vema katika shughuli za taasisi za kimazingira ili kutimiza

changamoto kuu mbili zinazohusiana:-

i. Umuhimu wa kuhifadhi mazingira ili yaweze kuchangia katika kuleta maendeleo endelevu

ii. Umuhimu wa kuwepo kwa usawa na uhakika katika upatikanaji wa njia za uzalishaji mali kwa watu maskini, na faida ambazo wanaweza kuzipata katika kuongeza fursa za jamii kujiongezea kipato, kujipatia huduma za afya, elimu na kupunguza uwezekano wa kuathiriwa na majanga ya kimazingira;

d) Onesha kwamba mkabala huu wa uhifadhi wa mazingira na kupunguza umaskini unahitaji mabadiliko ya kisera na kitaasisi katika sekta mbalimbali;uhusishaji wa watendaji wengi katika sekta ya umma,sekta binafsi na mashirika ya kijamii. Aidha, mkabala huu unahitaji ushiriki wa nchi zinazoendelea na zile zilizoendelea;

e) Onesha kwamba pamoja na mafanikio katika maeneo kadhaa, msukumo katika kuhifadhi mazingira unazidi kuongezeka duniani, ukiibua changamoto kuu katika matarajio ya kupunguza umaskini na kukuza maendeleo ya kiuchumi katika nchi zinazoendelea;

f) Onesha kwamba ubora wa mazingira na upatikanaji wa maliasili mbalimbali ni muhimu katika kuwawezesha watu maskini kujipatia riziki zao;

g) Jadili kuwa aina tofauti za kujipatia kipato ni muhimu kwani watu maskini wanahitaji kuwa na fursa mbalimbali ili kupunguza utegemezi kwenye maliasili pekee zinazopatikana kwenye maeneo yao.

**Kisanduku Na. 1.2:**
**Mifano ya uhusiano wa idadi ya watu, umaskini na mazingira**

Umaskini unaathiri idadi ya watu kutokana na:

- Kupungua kwa uwezo wa watu kupata maji safi na salama, kutafuta mbinu za kupunguza mahitaji ya nguvu-kazi kunaongeza haja ya kuzaa watoto ili wasaidie shughuli mbalimbali.
- Msingi mbovu wa rasilimali unaongeza haja ya kuzaa watoto wengi ili kufidia nguvu- kazi pale wengine wanapoumwa au kuzeeka.

- Ukosefu wa elimu unamaanisha mwamko mdogo wa njia za kupanga uzazi, hasa kwa wanawake. Hadhi ndogo ya wanawake inamaanisha kwamba wanamaamuzi madogo katika suala la uzazi.

Idadi ya watu inaongeza Umaskini kutokana na:

- Kuongezeka kwa ukosefu wa ardhi – maeneo yaliyorithiwa yanagawanywa na kugawanywa miongoni mwa watoto wanaozaliwa.
- Kuzisambaza kuliko kawaida huduma za kijamii, shule, vituo vya afya, vituo vya afya ya uzazi, maji na miundombinu ya maji-taka iliyopo.

Idadi ya watu inaathiri Mazingira kutokana na:

- Kuongeza matumizi ya ardhi, matumizi ya ardhi na misitu yaliyozidi mipaka, ufugaji wa mifugo uliopitiliza.
- Mmomonyoko wa udungo.
- Uhamiaji wa watu katika mitaa yenye msongamano, matatizo ya maji na mifumo ya maji-taka, hatari za taka za viwandani, uchafuzi wa hewa majumbani, miporomoko ya ardhi.

Umaskini kama sababu ya uharibifu wa mazingira kutokana na:

- Eneo dogo la kulifanyia mipango (linaloweza kufanyiwa kazi za kila siku za kuwezesha watu kuishi).
- Utegemezi wa kiwango cha juu wa vyanzo vya nishati isiyojadidika.
- Mtaji mdogo kwa ajili ya matumizi endelevu ya rasilimali (utegemezi kwa teknolojia duni).

Uharibifu wa mazingira kama chanzo cha umaskini, ni kutokana na:

- Rasilimali chache za kimazingira, hivyo kipato kidogo.
- Mazingira yaliyochafuliwa husababisha matatizo ya kiafya, hivyo uzalishaji mdogo.
- Kupungua kwa rutuba ya ardhi kunasababisha uzalishaji mdogo, na hivyo kipato kidogo.

***Viumbehai na maliasili.***

a) Onesha kwamba maliasili inaweza kuwa chanzo cha kujipatia riziki au kuongeza kipato na upatikanaji wa mahitaji muhimu ya kaya. Toa vielelezo kadhaa juu ya viwango vya utegemezi wa maliasili kwa watu maskini katika maeneo ya vijijini.

b) Taja na rejea data za matokeo ya tafiti yanayotoa ushahidi wa jinsi kaya maskini za vijijini zinavyojipatia kiasi kikubwa cha vipato vyao kutokana na maliasili.

c) Mambo mawili yanabainika katika machapisho mbalimbali:-
   - Watu maskini zaidi ndiyo hutegemea zaidi mazingira ili kupata kipato duni.
   - Lakini watu walio bora ndiyo hutumia zaidi maliasili ili kupata kipato bora.

d) Taja na jadili kwamba uharibifu wa maliasili unaathiri zaidi watu maskini. Onyesha hata hivyo kwamba, kuongezeka kwa kipato kunaongeza matumizi ya maliasili.

e) Toa ushahidi kwamba ukuaji wa uchumi hautapunguza msukumo wa kimazingira katika muktadha huu. Mfano unaweza kutolewa wa nchi zilizoendelea na nchi zenye kipato cha wastani.

f) Taja na jadili kwamba uharibifu wa maliasili na upoteaji wa viumbe anuwai vinapunguza upatikanaji wa riziki na mianya ya upatikanaji wa riziki kwa vizazi vijavyo vya watu maskini. Mifano inaweza kutolewa ya mifumo ya kilimo.

g) Uharibifu wa ardhi na vyanzo vya maji.

h) Upotevu wa mbegu za mazao na mifugo inayohimili wadudu na ukame ni tishio kubwa katika kuboresha uzalishaji wa kilimo ambao ni tegemeo la maisha ya watu wengi maskini waliopo vijijini, na ni muhimili wa mikakati ya kupunguza umaskini katika nchi nyingi.

i) Toa ushahidi kwamba watu maskini wanaathirika na uharibifu wa maliasili na upotevu wa viumbe anuwai zaidi ya watu ambao si maskini, kwa sababu ya rasilimali chache walizonazo na utegemezi wao mkubwa katika vyanzo vya kawaida vya kujipatia kipato.

j) Taja na jadili viumbe anuwai na huduma za mfumo wa ikolojia .

k) Onyesha kwamba mfumo wa ikolojia kama vile misitu, mifumo ya ikolojia ya kilimo, ukanda wa mbuga, maji safi na mifumo ya ikolojia

ya baharini (pamoja na miamba ya matumbawe) na viumbe anuwai vilivyomo ndani yake vinatoa mchango muhimu" unawezesha shughuli za uzalishaji mali.

## Kipindi cha Pili

### Kuhusianisha mazingira na umaskini

Wawezeshaji wajadili masuala yanayohusiana na umaskini na uhifadhi wa mazingira: ni jinsi gani mazingira na mabadiliko ya hali ya mazingira yanavyowaathiri watu maskini; wanaume, wanawake na watoto, katika viashiria vikuu vitatu vya umaskini wa watu:-

**a)** **Njia kuu za kuweza kuishi:** watu maskini hutegemea zaidi mazingira yao na maliasili na kwa hiyo, wanaathirika zaidi mazingira yanapoharibiwa au wanapopoteza uwezo wa kupata rasilimali;

**b)** **Afya:** watu maskini huathirika zaidi ardhi, maji na hewa wavutayo inapochafuliwa. Hatari za kimazigira ni mojawapo ya vyanzo vikuu vya magonjwa katika nchi zinazoendelea;

**c)** **Uwezekano wa kudhuriwa:** watu maskini wanaweza kuathirika zaidi maafa ya kimazingira na migogoro inayohusiana na mazingira. Pia wana uwezo mdogo wa kumudu na kuchukuliana na hali, pindi maafa ya kimaumbile na migogoro inapotokea.

- Mambo kadhaa kama haya yafuatayo yanaweza kutumika:-
  a. Mmoja kati ya watu watano duniani anaishi katika umaskini;
  b. Uwezo wa dunia kuwahifadhi watu bilioni 6 na kupata rasilimali wanazozihitaji ili kuishi unazidi kupungua;
  c. Mkutano wa Johannesburg wa 2002 ulikumbusha kwamba maendeleo endelevu ni muhimu katika kupunguza umaskini;
  d. Malengo ya Maendeleo ya Millennia na Mkakati wa NSGRP wa Tanzania unatambua umuhimu wa mazingira katika kuondoa umaskini;
  e. Bila uhifadhi wa mazingira ufaao haitawezekana kuzalisha chakula kinachohitajika kuondoa tatizo la njaa, kupunguza idadi ya watoto wanaokufa kwa magonjwa

yaambukizwayo kwa njia ya maji au kuondoa malaria katika hali yake ya sasa kama ugonjwa unaoua zaidi katika nchi za Afrika kusini mwa jangwa la Sahara.

**Kisanduku Na. 1.3**
**Mfano: Kuhifadhi njia za kujipatia riziki na mazingira nchini Tanzania**

1.1.2
Njia za kujipatia riziki zilikuwa katika hatari ya kupotea katika vijiji vya ukanda wa pwani wa mkoa wa Tanga nchini Tanzania kutokana na uvuvi usiokuwa endelevu, kushuka kwa thamani ya samaki waliovuliwa na usimamizi duni wa sheria. Shirika la misaada la Ireland na Shirika la uhifadhi wa Maliasili Duniani (IUCN) zilishirikiana na wananchi na mamlaka za mikoa na wilaya kwa zaidi ya miaka 10 ili kuwawezesha wananchi na taasisi kuhifadhi na kulinda rasilimali za baharini.

- Upunguzaji mkubwa wa mbinu haribifu za uvuvi;
- Uimarishaji wa hali ya miamba ya matumbawe na idadi ya samaki;
- Kuanzishwa kwa njia mbadala za kujipatia riziki (kama vile kilimo cha mwani);
- Wilaya kuendeleza kugharamia shughuli za uhifadhi rasilimali za pwani;
- Elimu ya mazingira kutolewa katika shule kwa ajili ya vizazi vijavvyo vya wavuvi;
- Sera za serikali zilizoboreshwa za uendelezaji wa uvuvi shirikishi.

**Ukuaji wa Uchumi na Mazingira**
Kuna mifano mingi ya jinsi usimamizi mbovu wa mazingira unavyoweza kudidimiza ukuaji wa uchumi.

Mwezeshaji afafanue uhusiano baina ya ukuaji wa uchumi na sera za mazingira na jinsi ambavyo uhusiano huo ni muhimu katika kupunguza umaskini; mwezeshaji atoe ushahidi kila inapowezekana.

Mwezeshaji asisitize yafuatayo:-

a) Nchi zinaweza kuwa na viwango vikubwa vya ukuaji wa uchumi na mbinu bora za uhifadhi wa mazingira. Hakuna mabadilishano sahili kati ya ukuaji wa uchumi na mazingira;

b) Kupuuza umuhimu wa mazingira katika ukuaji wa uchumi kunaathiri watu maskini kwa muda mfupi, na kunadidimiza kwa muda mrefu ukuaji wa uchumi na umadhubuti wake katika kupunguza umaskini;

c) Ubora wa kiwango cha ukuaji wa uchumi ni muhimu. Kimsingi ubora wa mambo yahusuyo ukuaji wa kiuchumi na mikakati ya sasa ya kuondoa umaskini unajengwa katika maeneo ya ukuaji wa kiuchumi.

d) Namna mbalimbali za ukuzaji wa uchumi zinaweza kuhusiana na athari tofauti tofauti za kimazingira.

**Kisanduku Na. 1.4**
**Mifano ya Usimamizi Mbovu wa Mazingira na Athari Zake Katika Ukuaji wa Uchumi**

- Kuporomoka kwa kilimo katika nchi nyingi kutokana na ardhi kuwa na chumvi iliyosababishwa na shughuli za kilimo cha umwagiliaji – kwa mfano, nchini Pakistani ambapo ilikadiriwa kwamba karibu asilimia 16 ya ardhi yake imeakuwa na chumvi chumvi kutoka katika visima vya kiwango cha chini na taratibu duni za umwagiliaji. Uharibifu huu unaigharimu nchi hiyo zaidi ya dola za Marekani milioni 200 kwa mwaka zinazotokana na uzalishaji mdogo (Benki ya dunia 1996b).
- Kuharibika kwa mapitio ya mito kunakotokana na kubadilika kwa matumizi ya ardhi katika vianzio vya mito hiyo – uhusiano baina ya matumizi ya ardhi katika vyanzo vya mito na mito hiyo kujaa michanga na mafuriko ni changamano sana; upo ushahidi wa mambo hayo kuhusiana. Kwa mfano, serikali ya China ilihitimisha kwamba mafuriko makubwa ya mwaka 1998 yalisababishwa kwa kiasi kikubwa na ukataji ovyo wa miti katika maeneo ya milima ya mto Yangtze (Benki ya dunia 2002d).

- Shughuli za ufugaji wa samaki kwa njia zisizo sahihi na uzalishaji wa uduvi ulisababisha magonjwa kutokana na njia duni za kuhifadhi mazingira nchini Taiwani na kusababisha hasara ya zaidi ya dola za Marekani bilioni moja katika Asia katika miaka ya 1990.

Wakati akitoa mifano hii, mwezeshaji afanye yafuatayo:-

a) Asisitize kwamba watu maskini wanapaswa kuchukuliwa kuwa sehemu ya suluhisho na si sehemu ya matatizo;

b) Asisitize kwamba juhudi za kuboresha mazingira katika namna ambayo itachangia maendeleo endelevu na kupunguza umaskini inapaswa kuanza kwa kuwapa kipaumbele watu maskini;

c) Aonyeshe kwamba katika sehemu nyingi sera zinaendelea kuelemea mawazo yasiyofaa juu ya watu maskini na uhusiano wao na mazingira;

d) Asisitize kwamba pia juhudi zinazofanywa na watu maskini kuhifadhi mazingira zinawapa changamoto watu wanaowalaumu maskini kwa kusababisha uharibifu wa mazingira na pia ni changamoto kwa sera zinazotunza mazingira kwa gharama ya maisha ya maskini.

**Uhifadhi wa Mazingira unavyochangia Maendeleo ya watu Maskini**

Maeneo manne ya kusisitizwa katika hili ni:-

**a)** **Njia za kujipatia kipato –** watu maskini hutegemea sana maliasili kupata chakula, malazi na kipato.

**b)** **Afya –** hali ya mazingira inachangia sehemu kubwa ya tishio la afya za watu maskini. Mazingira mabovu ya kiafya ndiyo husababisha hatari za kiafya kwa watu maskini. Shirika la Afya Duniani lilikadiria mwaka 2002 kwamba asilimia 21 ya mzigo wa gharama za matibabu duniani kote husababishwa na maafa ya kimazingira-- jumla ya siku zilizotumika katika ugonjwa na vifo vilivyosababishwa na magonjwa (WHO, 2002).

**c)** **Majanga ya asili –** watu maskini huwa na uwezekano mkubwa wa kuathiriwa na majanga ya kimaumbile, madhara ya mabadiliko ya

kimazingira na matatizo mengine ya kimazingira yanayoharibu njia za kujipatia riziki na upatikanaji wa chakula.

d) **Huduma za mifumo-ikolojia –** watu maskini wanategemea zaidi shughuli zinazofanywa katika mifumo-ikolojia kama vile delta, misitu ya mikoko, na maeneo ya hifadhi.

**Kisanduku Na. 1.5**
**Maeneo ya Hifadhi na Watu Maskini: utata katika uhifadhi wa mazingira?**

Malengo ya Maendeleo ya Millennia yanaelezea mafanikio katika kumaliza umaskini na pia kuhifadhi viumbe anuwai. Njia mojawapo ya kuhifadhi viumbe anuwai ni kwa kuanzisha maeneo ya hifadhi. Jamii ambazo hapo awali zilitegemea maeneo hayo ya hifadhi kama rasilimali zao zinaathirika kutokana na kuzipoteza rasilimali hizo, na hivyo kuzidisha umaskini kama, hatua zifaazo za kuwafidia zisipochukuliwa. Kupotezwa kwa rasilimali hizo kunaweza kusababisha mambo yafuatayo:

- Kupotea kwa kipato cha fedha zilizokuwa zikitokana na mauzo ya bidhaa zilizopatikana katika maeneo hayo yaliyohifadhiwa.
- Kupotea kwa bidhaa zilizopatikana moja kwa moja kutoka katika maeneo hayo yaliyohifadhiwa.
- Kupotea kwa ardhi ambayo sasa inaonekana kuwa ni sehemu ya hifadhi.

Mifano:

a) Hifadhi ya ziwa Mburo nchini Uganda jamii zinazozunguka hifadhi hiyo zililipwa na Mamlaka ya Hifadhi ya ziwa hilo kiasi cha dola za Marekani 230,000 kwa mwaka mmoja tu wa 1998 wakati hasara waliyoipata kutokana na uanzishwaji wa hifadhi hiyo inakadiriwa kufikia dola za Marekani 700,000. Hasara hiyo ilikuwa na uwiano wa 0.3 hivyo waliishi maisha duni sana wakati wa uwepo wa hifadhi hiyo kuliko walivyoishi kabla.

b) Serengeti magharibi nchini Tanzania wakazi wake walilipwa dola za Marekani 75,000 tu kati ya zote zilizopatikana katika utalii, lakini wakapata uharibifu wa hadi dola za Marekani milioni moja uliofanywa na wanyama pori, uwiano wa hasara waliyoipata ukiwa ni 0.07.

**Kisanduku Na. 1.6**
**Kunufaika kutokana na maeneo ya hifadhi**

Hitaji la msingi katika kupunguza migogoro na kuahakikisha kwamba kila upande una nia njema na uanzishwaji wa hifadhi ni kwa uwiano wa manufaa kwa pande zote husika kuwa kubwa kuliko ya jumla ya hifadhi.
Hii inamaanisha kwamba:-

a) Kuhakikisha maeneo ya hifadhi kwa ujumla yanafanyiwa tathmini ya hasara na faida zake;
b) Kuhakikisha gharama na faida zinagawanywa kwa jinsi ambayo kila upande unapata manufaa kutokana na kuwepo kwa hifadhi.

Utafiti wa hifadhi kubwa ya Panda nchini China unaonesha jinsi wakazi wanavyoweza kunufaika na uwepo wa hifadhi. Utafiti huu ulibainisha pande zote ambazo maslahi yake yanapaswa kuzingatiwa katika uanzishwaji wa hifadhi hiyo. Pande hizi zilikuwa ni: (a) watalii wa hifadhi ya Panda, (b) watalii wa China ambao walikuwa radhi kuchangia kifedha uanzishwaji wa hifadhi ya Panda, lakini hawakuwa na mpango wa kuitembelea hifadhi hiyo, (c) wahifadhi, wanaharakati wa ndani na nje wa uhifadhi, (d) jamii ziishizo kuzunguka maeneo ya hifadhi na wakulima maskini ambao walipaswa kupoteza ardhi zao kutokana na shughuli za uhifadhi, na (e) waangalizi wa hifadhi waliolipwa mshahara mdogo ambao walikuwa na jukumu la kuwalinda Panda hao ambao walichukiwa sana na wakulima. Uchunguzi makini wa utayari wa watalii kuchangia shughuli za uhifadhi kwa

(a) kupandisha ada ya kuingia katika hifadhi na (b) kulipia stempu ya Panda kwenye hati za kusafiria zilizotolewa na serikali ulionyesha kwamba kiasi kikubwa cha mamilioni ya dola kingeweza kukusanywa kila mwaka. Bajeti ya karibuni ya hifadhi ilikuwa ni dola robo milioni kwa mwaka. Kwa kuwa watalii walikuwa radhi kulipia, hakukuwa na matatizo makubwa: faida waliyoipata ni kutambuliwa kwamba walichangia katika uanzishwaji wa hifadhi ya Panda.

Wanaharakati wa mazingira wangewezeshwa zaidi kutokana na mfuko wa hifadhi. Tafiti pia zilionyesha kwamba watalii walikuwa radhi kuchangia malipo ya ziada wakijua kwamba malipo haya yatatumika kuwafidia wakulima walioishi katika maeneo hayo. Kwa hiyo hata wakulima wangenufaika. Mwisho, fedha hizo zingewezesha waangalizi wa hifadhi kulipwa mishahara mizuri zaidi wakati ambapo fidia kwa wakulima ingeondoa chuki walizokuwa nazo wakulima hao dhidi ya waangalizi wa hifadhi. Hifadhi zinazozingatia maslahi ya wote, huwanufaisha pia watu maskini.

Kuzifanya pande mbalimbali kukubaliana na mipango kama hiyo si jambo rahisi. Hatua ya kwanza ni kubainisha wadau wote. Hatua ya pili ni kuhakikisha kuwa kuna malipo ya namna fulani yatakayozinufaisha pande zote. Katika kuzingatia dhamira kuu ya taarifa hii, mgao wa faida unapaswa kuelemea uanzishwaji wa rasilimali mpya. Kugawana mapato tu hakuwezi kufidia kwa uhalisia upotevu wa rasilimali kwa wanajamii waishio katika maeneo husika. Haitawezekana kila mara kutenga faida kwa namna hii, na inawezekana zaidi kama kuna spishi au mfumo wa ikolojia za kipekee, kwa sababu kuna uhakika wa mapato pindi hifadhi itakapoanzishwa. Lakini kanuni za kugawana faida hazina budi kuzingatiwa.

**Jedwali Na. 1.1: Maeneo ya msingi yanayohitaji uandaaji wa sera ili kuboresha matokeo ya mahusiano ya umaskini na mazingira.**

| | |
|---|---|
| Kuboresha utawala | • Ambatanisha mambo yahusuyo umaskini na mazingira na mipango ya maendeleo ya taifa<br>• Imarisha ugawanaji wa majukumu katika uhifadhi wa mazingira<br>• Yape uwezo mashirika ya kijamii, na hasa ya watu maskini na waliotengwa<br>• Zingatia mahusiano ya kijinsia katika mahusiano ya umaskini na mazingira<br>• Imarisha juhudi za kupambana na ufisadi katika kuhifadhi mazingira<br>• Kupunguza migogoro inayohusiana na mazingira<br>• Boresha usimamizi na tathmini ya mahusiano ya umaskini na mazingira. |
| Kuboresha rasilimali za watu maskini | • Imarisha haki za watu maskini kumiliki rasilimali<br>• Saidi uwezo wa watu maskini kuhifadhi mazingira<br>• Panua upatikanaji wa teknolojia rafiki kwa mazingira husika<br>• Punguza uwezekano wa maskini kudhuriwa na mazingira. |
| Kuboresha ukuaji wa uchumi | • Unganisha mambo yahusuyo mahusiano ya umaskini na mazingira na mabadiliko ya sera za kiuchumi<br>• Ongeza matumizi ya thamani ya mazingira<br>• himiza ushirikishwaji wa sekta binafsi zinazohusika katika uhifadhi wa mazingira ya watu maskini<br>• fanya mabadiliko muhimu ya sera zihusuzo mazingira ya watu maskini |
| Kufanyia mageuzi sera za kimataifa na kuleta mageuzi ya kiviwanda | • fanyia mageuzi sera za kimataifa na kiviwanda za biashara za nchi<br>• fanya uwekezaji wa moja kwa moja toka nje kuwanufaisha maskini na kulinda mazingira<br>• saidia michango ya mikataba ya kimataifa ya uhifadhi wa mazingira katika kupunguza umaskini<br>• himiza uzalishaji na matumizi endelevu<br>• himiza ufanisi wa mashirika ya maendeleo na msamaha wa madeni. |

Chanzo: WB (2002) Kuhusianisha Harakati za Kupunguza Umaskini na Utunzaji wa Mazingira: Changamoto na Mafanikio ya Sera

***Maswali ya mjadala***

a) Je, uhusiano wa masuala ya umaskini na mazingira utaingizwaje katika mipango ya maendeleo ya taifa?
b) Ni kwa jinsi gani tunaweza kugawanya majukumu ya shughuli za uhifadhi wa mazingira?
c) Ni kwa jinsi gani tunaweza kuyapa nguvu mashirika ya kijamii na hasa yale yafanyayo kazi kwa ajili ya watu maskini na waliotengwa?
d) Ni kwa jinsi gani tunaweza kubainisha masuala ya uhusiano wa umaskini na mazingira kijinsia?
e) Ni kwa jinsi gani tunaweza kuimarisha vita dhidi ya ufisadi katika uhifadhi wa mazingira na haki za watu maskini?
f) Ni kwa jinsi gani tunaweza kudhibiti na kutathmini uhusiano bora wa umaskini na mazingira?
g) Ni kwa jinsi gani tunawawezesha watu maskini kuhifadhi mazingira yao?
h) Ni kwa jinsi gani tunaweza kupunguza uwezekano wa watu maskini kudhuriwa na majanga ya kimazingira?
i) Ni kwa jinsi gani tunaweza kuingiza masuala ya mazingira katika mabadiliko ya sera za kiuchumi?

**Marejeo**

Nanyayaran, D, R. Patel, K. Schafft, A. Rademacher and S. Koch-Schulte. 2000. Voices of the Poor: Can ANYONE Hear Us? Oxford University Press, New York

Thomas V., M. Dailami, A. Dhareshwar, D. Kaupfmann, N. Kishor, R. Lopez na Y. Wang. 2000. The Quality of Growth, Oxford University Press.

Thulow, J na P. WOBST 20006. “Not All Growth is Equally Good for the Poor: The Case of Zambia” *Journal of African Economies*,

Volume 15, Number 4, pp. 603 – 625 December.

United Nations. 1992. *Earth Summit Agenda 21: The United Nations Programme of Action From Rio*, United Nations, New York

URT. 2008 b. "2007 Household Budget Survey Preliminary Data" National Bureau of Statistics, Dar es Salaam, September.

# MODULI YA PILI:

## Utawala na Mchakato wa Sera za Nchi

**Malengo ya Moduli**

Katika moduli hii washiriki wataelekezwa masuala kadhaa ya kiutawala yanayohusu uhifadhi wa mazingira na upunguzaji wa umaskini. Pia washiriki wataelimishwa kuhusu sera na mikakati mbalimbali na umuhimu wake katika kupunguza umaskini na kuhifadhi mazingira. Moduli hii inakusudiwa kuwasaidia washiriki kuelewa masuala ya utawala na jinsi yanavyohusiana na uhifadhi wa mazingira na kupunguza umaskini.

**Muda uliopendekezwa kutumika**

Muda usiozidi masaa matatu utatumika kuwasilisha na kupitia masuala ya kipengele hiki. Hii itajumuisha angalau dakika 30 za mawasilisho ili kuwawezesha washiriki kuelewa hali halisi nchini Tanzania._

**Njia za ufundishaji**

Matumizi ya njia zaidi ya moja yatafaa katika kufundishia moduli hii. Njia zinazopendekezwa kutumika ni pamoja na mihadhara, kazi za vikundi, mijadala na mifano hai. Njia hizi zitawawezesha washiriki kushirikiana miongoni mwao.

**Kipindi cha kwanza**

**Utawala na Uhifadhi wa Mazingira**

Mwezeshaji asisitize umuhimu wa utawala na jinsi unavyoweza kuathiri uhifadhi wa mazingira na kupunguza umaskini:-

a) Jinsi gani utawala bora unaweza kupatikana.
b) Mchango wa utawala bora katika kuleta uhifadhi endelevu wa mazingira na kupunguza umaskini.

Baadhi ya mambo yanayoweza kujumuishwa katika mjadala ni pamoja na:-

i) Ushiriki wa watu maskini na makundi yaliyotengwa katika michakato

ya maandalizi ya sera na mipango ni muhimu ili kuhakikisha kwamba masuala muhimu ya kimazingira yanayowaathiri yanashughulikiwa ipasavyo. Lengo linapaswa kuwa kujenga uwezo wa watu masikini kupata taarifa zinazohusu mazingira ili kukuza uwazi na uwajibikaji.

ii) Haja ya kuimarisha mfumo wa mahakama kama taasisi huru ili kusaidia ushiriki wa taasisi na asasi za kiraia katika kusuluhisha migogoro.

iii) Majukumu na uhusiano wa kijinsia katika masuala ya uhifadhi wa mazingira na upatikanaji wa rasilimali za kimazingira ni kigezo muhimu kinachopaswa kuzingatiwa.

**Kuimarisha juhudi za kupambana na ufisadi ili kuwasaidia wananchi maskini na kuhifadhi mazingira**

Mwezeshaji asisitize yafuatayo:-

a) Ufisadi ni tatizo kubwa katika utawala na maendeleo, na kwamba linasababisha usimamizi mbovu wa mazingira, hasa katika uvunaji holela wa maliasili, udhibiti wa uchafuzi wa mazingira, n.k. Kielelezo cha mazingira endelevu (Kisanduku Na. 2.1) kinabainisha kwamba ufisadi unachangia kwa kiasi kikubwa katika usimamizi mbovu wa mazingira.

b) Uandaaji, utoaji na usambazaji mzuri wa taarifa zinazofaa, mfumo unaofaa wa kisheria pamoja na matumizi ya vikwazo vinavyoweza kupunguza matumizi yasiyo endelevu ya rasilimali.

**Kisanduku Na. 2.1 Mfano: Mfumo wa usimamizi wa mazingira na uzingatiaji wa sheria nchini Tanzania**

Kama ilivyo kwa nchi nyingi zinazoendelea ambazo zina utajiri mkubwa wa maliasili, Tanzania inakabiliana na changamoto za kiutawala, hasa katika kuweka mipango juu ya umiliki na matumizi ya maliasili hizi. Kwa mfano, ripoti ya hivi karibuni inakadiria kwamba mapato ya serikali kutokana na mazao ya misitu yanapatikana kupitia usafirishaji

wa magogo katika mikoa ya kusini mwa Tanzania ni kati ya asilimia 4- 15 tu, (Milledge, Gelvas, na Ahrends 2007). Ripoti hii, pamoja na vichwa vya habari vya magazeti vinavyofichua usafirishaji haramu wa magogo kwenda nje ya nchi vimeibua mijadala na kuchagiza kuwepo kwa juhudi za ziada za serikali na nchi wafadhili kulishughulikia tatizo hili la uwezo mdogo wa ukusanyaji mapato kutoka katika mazao ya misitu. Umakini pia umewekwa katika maeneo mengine yenye usimamizi duni wa rasilimali za mazingira, ikijumuisha udhibiti mdogo wa uvuvi haramu (mfano: matumizi ya mabomu, makokoro na sumu) na uwindaji haramu. Kuweka msisitizo katika changamoto katika utawala wa kimazingira, Tanzania imefanikiwa kubainisha mahusiano ya umaskini na mazingira katika mkakati wa kupunguza umaskini pamoja na kutenga fedha kwenye bajeti ili kufikia malengo mahsusi ya sekta hii.

**Mchango wa Mashirika ya Maendeleo katika Utawala**

Mwezeshaji asisitize umuhimu wa mashirika ya maendeleo na masuala muhimu yanayotakiwa ili kuboresha utawala. Aidha, umuhimu wa harakati za masuala ya mazingira katika ushirikiano wa kimaendeleo ngazi ya jamii na taifa pamoja na vipaumbele visisitizwe. . Wakati nchi zinazoendelea zina kazi kubwa ya kufanya kuondoa ufisadi, nchi zilizoendelea pia zina wajibu wa kusaidia. Hii ni kwa sababu ama zinaweza kuwa kimbilio la mafisadi au zinaweza kuhamasisha vitendo vya aina hiyo. Hivyo ushirikiano wa kimataifa ni muhimu kwenye hifadhi ya mazingira.

**Kipindi cha Pili**

Usimamizi wa Mazingira Asilia

Mwezeshaji asisitize umuhimu wa mambo yafuatayo:

a) Kuingiza masuala ya mazingira katika mikakati ya kupunguza umaskini na mipango mingine ya kitaifa ya kimaendeleo.

b) Kuimarisha utawala katika mambo yanayohusu mazingira – hii inajumuisha kuimarisha taasisi za wakazi wa maeneo husika na

kuwashirikisha katika haki zao na umiliki wa maliasili na katika uhifadhi wake.

c) Kuimarisha uwezo wa serikali kusimamia, kutunga sheria na kudhibiti mazao ya maliasili.

d) Kuwawezesha na kuwavutia watu maskini kuwekeza katika utoaji wa huduma za umma. Hii inajumuisha upendeleo katika utoaji wa huduma za mikopo na za kibiashara katika maeneo ya hifadhi, na hatua za kuhimiza usawa katika umiliki na upatikanaji wa rasilimali kama za maji na mazao ya misitu.

e) Kuwezesha mashirika ya maendeleo kupata rasilimali zaidi na hakikisha kwamba kiasi kikubwa cha rasilimali hizi kinatumika katika shughuli za utunzaji wa mazingira na kupunguza umaskini.

f) Kujenga na shirikiana na mitandao na jumuiya mbalimbali ili kubainisha na kushughulikia uhusiano uliopo baina ya mazingira na upunguzaji wa umaskini. Washirika wa shughuli hizi wanapaswa kuwa mashirika ya maendeleo, taasisi za elimu, asasi zisizo za serikali (AZISE), na mashirika ya kijamii katika nchi zilizoendelea na zile zinazoendelea.

**Jedwali 2.1: Hatua za Kushughulikia Masuala ya Mazingira**

| ***Awamu ya maandalizi*** **Kubainisha tatizo: Uhusiano wa Umaskini na Mazingira** | ***Awamu ya 1:*** **Kuingiza masuala ya mazingira katika mikakati ya maendeleo ya nchi** | ***Awamu ya 2:*** **Kujenga uwezo wa utekelezaji** |
|---|---|---|
| Tathmini ya awali | • Ushahidi mahsusi kwa nchi husika<br>• Kuingiza tathmini ya mfumo-ikolojia<br>• Uchambuzi wa kiuchumi | • Udhibiti wa umaskini na mazingira<br>• Vigezo na ukusanyaji wa takwimu |
| Bainisha uhusiano wa msingi baina ya umaskini na mazingira | | |

| | | |
|---|---|---|
| Onesha umuhimu wa uhusiano wa kimazingira na umaskini | • Kuchochea michakato ya uundaji wa sera<br>• Michakato ya kitaifa –MKUKUTA/ Malengo ya Milenia<br>• Michakato ya kisera na ya wakazi wenyewe | • Kubajeti na kugharamia utunzaji wa mazingira<br>• Michakato ya kupanga bajeti na njia za ugharimiaji |
| • Kuhamasisha umma na kukuza weledi.<br>• Makubaliano ya kitaifa na dhamira ya kweli. | Uingiliaji kati wa kisera na uanzishwaji wa programu, mikakati na mageuzi ya kisera | • Utekelezaji wa sera na programu<br>• Utekelezaji wa kisekta na wa kijamii |
| Tathmini ya mahitaji ya kitaasisi na ya kuja uwezo | • Maendeleo ya kitaasisi na ya kiuwezo<br>• Kuongeza uwezo wa kimkakati | • Maendeleo ya kitaasisi na kiuwezo<br>• Kuimarisha hali ya baadaye |

Vyanzo: UNDP/UNEP (2006) Guidance Note on Mainstreaming

**Vipengele vya Kisera vinavyohusianisha na umaskini na mazingira**

Kimsingi kuna makundi makuu mawili ya mbinu zinazoweza kutumika katika utekelezaji wa sera. Mbinu hizi ni:

a) Mbinu zinazoelemea soko (MBIs) - zinatumia mabadiliko ya bei kutoka katika bei za kawaida.

b) Mbinu za kuamuru na kudhibiti (Command and Control-CAC)- ambazo zinaongoza mahusiano ya mdhibiti na mdhibitiwa.

**Mbinu zinazoelemea soko (Market Based Instruments-MBIs)**

Wakati mwingine hizi huitwa mbinu za kiuchumi kwani zinaathiri gharama na faida ya mbinu nyingine ambazo zingetumiwa na mashirika ya maendeleo, na hatimaye kuwa mazoea kwa jinsi ambayo iliyokusudiwa kukubalika na mazingira. Kwa maneno mengine, mbinu hizi zinaitwa za kiuchumi kwa sababu zinahusu masuala ya kibiashara kwa kubadilisha gharama ya kawaida iliyozoeleka na mashirika ya kimataifa. Mbinu hizi

zinapatikana kwa wingi katika machapisho, yaani:

a) Kutozwa faini kwa kuchafua mazingira: malipo ya moja kwa moja kwa wachafuzi wa mazingira;
b) Gharama za watumiaji: malipo ya huduma za umma kama vile ukusanyaji taka na uhifadhi wa maji-taka;
c) Gharama za bidhaa: gharama zinazotozwa bidhaa zinazosababisha uchafuzi wa mazingira wakati wa utengenezaji wake, utumiaji au mabaki yake baada ya matumizi;
d) Malipo ya maliasili: malipo ya matumizi ya maliasili kama vile uchimbaji wa madini, mafuta, maji na matumizi ya rasilimali anuwai;
e) Mfumo wa kuweka na kulipa fidia: ada/malipo yanayofanywa wakati wa kununua bidhaa. Malipo yanarudishwa pale bidhaa iliyotumika inaporejeshwa au kifaa chake cha kuhifadhia kitakaporudishwa;
f) Ushuru wa kukiuka masharti: ushuru kwa wachafuzi wa mazingira wanaoshindwa kutekeleza sheria fulani (kwa mfano faini, adhabu n.k.);
g) Ruzuku: namna zote za misaada ya kifedha kwa watunzaji wa mazingira au watumiaji wa maliasili (kwa mfano, misaada, mikopo nafuu, misamaha ya kodi);
h) Kodi za mazingira: kodi inayotozwa kwa kila shughuli na pia inaweza kuhusishwa na kiasi cha uzalishaji au gharama za uzalishaji.

MBIs zinaathiri gharama za kawaida (gharama ya uzalishaji- faida ya uzalishaji) ambazo shughuli za uchumi hukabiliana nazo. Gharama za kawaida huathiri muelekeo wa maamuzi yanayofikiriwa na wawandaaji wa sera.

Mbinu za kiuchumi zinahitajika kugawanywa katika makundi makuu mawili: makundi haya ni:

**Tozo za mazingira:**

a) Kundi hili linajumuisha aina zote za kodi na gharama za mtumiaji pamoja na mfumo wa kuweka na kulipa. Kundi hili ndilo lililo maarufu zaidi hata katika nchi zinazoendelea.

**Vibali/mikopo ya biashara:**

b) Kwa kawaida huanzishwa ili kukabiliana na matatizo ya haki miliki. Watu wenye vibali wanaweza kubadilishana vibali hivyo kulingana na tofauti katika miundo ya gharama za uzalishaji.

**Mbinu za kuamuru na kudhibiti**

Kundi hili la mbinu za sera za mazingira ni pana na linajumuisha sheria na taratibu za:-

a) Kiwango cha juu kinachoruhusiwa katika uzalishaji,

b) Marekebisho katika mchakato na/au vifaa,

c) Marufuku, ugawaji wa kanda n.k. Wakati mwingine taratibu hizi huwekwa kama vile:

- viwango vya tekinolojia: kiwanda hakiko huru kuchagua hatua za kuboresha mazingira
- viwango vya uzalishaji: kiwanda kinaweza kuchagua tekinolojia ya kutumia mradi tu ina uwezo wa kutoa bidhaa za kiwango kilichowekwa.

**Jedwali 2.2: Uainishaji wa mbinu za sera za mazingira**

| Taratibu za kulazimisha na kudhibiti | Mchango wa moja kwa moja wa serikali | Kuzihusisha sekta binafsi na za umma | Kutumia soko | Kujitafutia masoko |
|---|---|---|---|---|
| •• viwango<br>•• marufuku<br>•• vibali na mafungu (*Quotas*)<br>•• ugawaji wa kanda<br>•• dhima<br>•• fidia ya kisheria<br>•• taratibu zinazo badilika badilika | ••miundombinu ya mazingira<br>•• kanda au maeneo ya kiuchumi na kibiashara<br>•• mbuga za wanyama, hifadhi za taifa, na maeneo ya starehe<br>•• ukarabati wa mfumo wa ikolojia | •• ushirikishwaji wa umma<br>••ugawaji wa majukumu<br>•• utoaji wa taarifa<br>•• uwekaji wa lebo za kiuchumi<br>•• makubaliano ya hiyari<br>•• ushirika wa taasisi za umma na za binafsi | •• kukomesha ruzuku zisizostahili<br>••kodi na ushuru wa mazingira<br>•• gharama za mtumiaji<br>•• mifumo ya kuweka na kurudishiwa<br>•• ruzuku zilizokusudiwa<br>•• udhibiti binafsi (kama vile ISO 14000) | •• haki miliki<br>•• vibali na haki zinazobadilishika<br>•• programu mpya<br>•• manunuzi yanayohitajika<br>•• mifuko ya mazingira na ya uwekezaji<br>•• mifuko ya mbegu na upendeleo<br>•• ulipaji wa gharama za huduma za mifumo ya ikolojia |

**Sera na Mikakati**

Mwezeshaji anapaswa:

a) Kutoa ushahidi kutoka katika mikakati ya kitaifa, vipaumbele na sera za kupunguza umaskini jinsi zinavyohusiana na mazingira.

b) Kutoa orodha ya sera za mazingira na kisekta zinazohusiana na mazingira.

Mifano:

**Sera ya Taifa ya Mazingira (1997)**

Mwezeshaji anapaswa kuwasilisha vipengele muhimu vya sera hii:

a) Inabainisha kuwa maendeleo endelevu ni suala la msingi katika sera ya taifa ya utunzaji wa mazingira.

b) Inaonyesha dhamira ya dhati ya serikali kuhusu maendeleo endelevu katika vipindi vyote.

c) Inabainisha matatizo sita ya kimazingira ambayo ni ya msingi.

d) Inazingatia uhusiano baina ya umaskini na mabadiliko ya idadi ya watu kama sababu kuu inayochangia uharibifu wa mazingira nchini.

**Sheria ya Usimamizi wa Mazingira (2004)**

Sheria inatambua masuala ya mifumo ya ikolojia na uhifadhi wa mazingira kama inavyobainika hapa chini:

**a)** **Kifungu cha 18** ya sheria inatoa uwezo wa kufanya ukaguzi utakaosaidia uhifadhi mzuri wa mazingira, kufanya na kuratibu tafiti, uchunguzi na ukaguzi wa mazingira, kukusanya na kusambaza taarifa kuhusu matokeo ya tafiti, kuchapisha na kusambaza vitini, miiko au miongozo ya uhifadhi wa mazingira na ya kuzuia uharibifu wa mazingira.

**b)** **Kifungu cha 47** ya sheria inatoa mamlaka kwa waziri mwenye dhamana ya mazingira kulitangaza eneo lolote lenye maliasili ya kipekee kuwa hifadhi ya taifa.

**c)** **Kifungu cha** 48 ya sheria inatoa uwezo wa kuwezesha tafiti za kisayansi kwa ajili ya kuendeleza jitihada za uhifadhi wa mazingira na kuendeleza mipango ya mifumo ya ikolojia ya maeneo ya hifadhi.

d) **Kifungu cha** 55 ya sheria inatoa mamlaka ya kutoa miongozo na kutathmini hatua za utunzaji wa fukwe za bahari, mito na maziwa.

e) **Kifungu cha 58** inatoa uwezo wa kubainisha na kutunza milima, miinuka na maeneo yaliyo katika hatari ya kuharibiwa.

f) **Kifungu cha** 108 ya sheria inatoa uwezo wa kufanya tafiti juu ya hali ya sasa ya kitekinolojia ili kuinua juhudi za pamoja za kuzuia uchafuzi wa mazingira, udhibiti na ufuatiliaji wa maendeleo ya kitekinolojia katika kuzuia na kupunguza uchafuzi wa mazingira unaosababishwa na taka zitokanazo na tekinolojia hizo.

g) **Kifungu cha 173** ya sheria inatoa uwezo wa kukusanya na kuchambua takwimu zilizopo na taarifa zihusuzo mazingira na maliasili na kusambaza taarifa kwa watumiaji wa umma na binafsi na tume ya tafiti ya mazingira na athari za mazingira katika masuala ya maendeleo.

h) **Kifungu cha 174** inatoa uwezo wa kuanzisha na kuendeleza mfumo mkuu wa taarifa za mazingira ambao utahifadhi matokeo ya tafiti mbalimbali, data na takwimu zilizotolewa na taasisi za umma au za binafsi katika uhifadhi na usimamizi wa mazingira.

i) **Kifungu cha 177 ya** sheria inatoa uwezo wa kukagua na kutafiti juu ya hali ya mazingira na kutabiri mabadiliko ya mazingira na tafiti nyingine zinazoweza kusaidia katika uandaaji wa sera na mikakati ya uhifadhi na utunzaji wa mazingira.

**Sera za kisekta**

Mwezeshaji anapaswa kujadili kwa ufupi sera za kisekta kwa lengo la kuonesha ni jinsi gani masuala ya mazingira na kupunguza umaskini yalivyoshughulikiwa.

Masuala ya mazingira yanashughulikiwa katika namna mbalimbali ikiwa ni pamoja na:

a) Ushiriki wa sekta nyingine katika uhifadhi na usimamizi wa mazingira

b) Ushirikishwaji wa wanawake na makundi mengine ya jamii katika shughuli za uhifadhi wa mazingira.

c) Uendelezaji wa tekinolojia rafiki kwa mazingira na mifumo-ikolojia endelevu.

d) Uanzishaji na utekelezaji wa tathmini ya athari kwa mazingira (EIA) katika miradi ya maendeleo kama mbinu muhimu; na

e) Utumiaji wa kanuni ya mchafuzi kulipa kama mbinu ya kiuchumi katika kudhibiti uchafuzi na kuhakikisha kuwepo kwa hewa safi na vyanzo bora vya maji na usimamizi wa maji-taka.

Sera zinazohusiana na mazingira ni pamoja na:

i. Sera ya Ardhi;
ii. Sera ya wanyama pori;
iii. Sera ya Madini;
iv. Sera ya Misitu;
v. Sera ya Uvuvi;
vi. Sera ya Kilimo na Mifugo;
vii. Sera ya Utalii;
viii. Sera ya Maendeleo endelevu ya Viwanda;
ix. Sera ya Nishati;
x. Sera ya Maji;
xi. Sera ya Ujenzi;
xii. Sera ya Usafirishaji;
xiii. Sera ya Afya;
xiv. Sera ya Mifugo ; na
xv. Sera ya Maendeleo ya Makazi.

## Kipindi cha Tatu

## Kujumuisha Masuala ya Mazingira katika Mikakati ya Kupunguza Umaskini Nchini Tanzania

Mwezeshaji anapaswa kuanza kipindi hiki kwa kutoa fasili ya dhana ya uingizwaji wa masuala mtambuka katika mikakati ya kuondoa umasikini, na kisha aendelee kwa kubainisha kwamba mikakati ya awali haikuzingatia sana masuala ya mazingira kama inavyojibainisha katika MKUKUTA kuanzia mwaka 2000. Pia, abainishe kwamba ingawa serikali imetambua umuhimu wa mazingira na imejumuisha masuala ya mazingira katika michakato mingi muhimu, changamoto kuu inabaki kuwa ni kwa jinsi gani serikali itawekeza

katika usimamizi wa mazingira ili kuleta maendeleo na kupunguza umaskini kama ilivyopangwa katika Dira ya Maendeleo ya 2025.

**Ujumuishaji wa mazingira katika mipango ya kitaifa**

Dhana ya ujumuishaji katika muktadha huu inamaanisha kuingiza masuala ya mazingira katika mipango na bajeti katika ngazi tofauti kama vile:

a) Wizara, mashirika na idara
b) Serikali za mitaa (LGAs)
c) Ugawaji wa rasilimali
d) Mapitio ya matumizi ya umma

**MKUKUTA na Mazingira**

**Malengo ya mazingira katika MKUKUTA**

Pitia kwa ufupi makundi yaliyopo katika MKUKUTA

**Eneo la 1: Maendeleo na kupungua kwa umaskini wa kipato**

Maendeleo makubwa na yaliyo na usawa yanapatikana na kuendelezwa

**Eneo la 2: Ubora wa maisha na ustawi wa kijamii**

a) Ubora wa maisha na ustawi wa kijamii, kwa kuzingatia sana uboreshaji wa hali za watu maskini na makundi yaliyo katika hatari.
b) Kupunguza kutokuwepo kwa usawa katika matokeo (mfano: elimu, njia za kuishi, afya) katika jiografia, kipato, umri, jinsia na makundi mengine.

**Eneo la 3: Utawala na uwajibikaji**

a) Kuongezeka kwa amani, utulivu wa kisiasa, umoja na mshikamano wa kitaifa
b) Demokrasia na uvumilivu wa kisiasa na kijamii
c) Utawala bora na utawala wa sheria

Uwajibikaji wa viongozi na watumishi wa umma.

Mwezeshaji abainishe malengo yanayohusu mazingira yaliyopo katika MKUKUTA

a) Kupunguza kuathirika kwa mazingira na vyanzo vya watu kujipatia riziki.
b) Kuongezeka kwa mchango wa uvuvi na misitu katika kipato cha wakazi wa vijijini.
c) Kupunguza uharibifu wa mazingira na upoteaji wa viumbe anuwai.
d) Kuhifadhi maliasili na mifumo ya ikolojia inayotegemewa na watu katika shughuli za uzalishaji mali.
e) Kupunguza taka hatari za viwandani na kwenye mifereji ya umwagiliaji mashambani.
f) Kuboresha utupaji wa taka kwa 95% kufikia mwaka 2010 na kupunguza uwezekano wa kudhurika na majanga ya kimazingira.
g) Kupunguza uwezekano wa watu kuathiriwa na majanga ya asili.

Katika mjadala, bainisha baadhi ya malengo ya kimazingira yaliyo wazi yaliyopo katika MKUKUTA, ukizingatia kwamba kati ya malengo 108 ya MKUKUTA, zaidi ya malengo 15 yanahusiana moja kwa moja na mazingira na maliasili, na katika malengo mengine mengi malengo yanategemewa kusaidia katika kutimizwa kwa malengo hayo.

Mwingiliano kati ya malengo ya kudhibiti uchafuzi wa mazingira, kupunguza vifo vya akina mama wajawazito na watoto wadogo, lishe duni na magonjwa.

Uhusiano baina ya mazingira, ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini wa kipato unasawiriwa sana katika mikakati ya malengo ya kundi la kwanza. Kwa mfano, chini ya lengo la kusaidia kupatikana kwa ukuaji mpana wa uchumi ambao ni endelevu, kuna mkakati wa kukuza pato la taifa kwa 6-8% kufikia mwaka 2010. Katika kufanikisha hili MKUKUTA unaingilia kati, katika utunzaji wa mazingira na usimamizi endelevu wa vyanzo vya maji ili kuhakikisha upatikanaji wa huduma za maji na nishati kwa ajili ya shughuli za kiuchumi na watu.

La muhimu zaidi ni kwamba uingiliaji kati, katika uhifadhi wa mazingira unatarajiwa kuchangia kufanikishwa kwa malengo yaliyopo katika kundi la 3 linalohusu utawala na uwajibikaji. Kwa mfano, kuna uingiliaji katika umiliki na udhibiti wa mazingira na maliasili, na katika juhudi za kupunguza ufisadi kwenye sekta za maliasili (mfano, usafirishaji haramu wa magogo).

**Jedwali la 2.3 Muhtasari wa malengo maalumu yanayohusiana na mazingira yaliyomo kwenye MKUKUTA**

| **ENEO LA 1: UKUAJI WA KIPATO NA UPUNGUZAJI WA UMASKINI WA KIPATO** | |
|---|---|
| **Malengo** | **Mikakati** |
| 2. Kusaidia ukuaji wa uchumi na maendeleo endelevu. | • Kupungua kwa athari katika mazingira na kwa maisha ya watu.<br>• Kupungua kwa uharibifu wa ardhi na viumbe anuwai. |
| 4. Kupunguza umaskini wa kipato kwa wanaume na wanawake waishio vijijini | • Ongezeko la michango inayotoka katika sekta za wanyamapori, misitu na uvuvi katika pato la jamii za vijijini. |
| **ENEO LA 2: UBORESHAJI WA MAISHA NA HALI YA KIJAMII** | |
| **Malengo** | **Mikakati** |
| 3. Jamii inaweza kupata maji safi na salama, usimamizi bora wa maji-taka, makazi bora na mazingira salama na endelevu, na kwa jinsi hiyo kupunguza uwezekano wa kudhurika na maafa ya kimazingira. | • Kuongeza idadi ya wakazi wa vijijini wapatao maji safi na salama kutoka asilimia 53 mwaka 2003 hadi asilimia 80 mwaka 2009/10 na kupunguza kwa muda unaotumiwa na katika kutafuta maji. Na kutoka asilimia 73 hadi asilimia 90 kwa wakazi wa mijini katika kipindi hicho hicho.<br>• Kuongeza idadi ya watu wanaotumia mifumo ya maji-taka kutoka asilimia 17 mwaka 2003 hadi asilimia 30 mwaka 2010 katika maeneo ya miji husika.<br>• Kupunguza idadi ya kaya ziishizo katika makazi duni yasiyokuwa na huduma muhimu za kijamii. |

| Malengo | Mikakati |
|---|---|
| | • Asilimia 100 ya shule ziwe na mfumo bora wa maji-taka kufikia mwaka 2010.<br>• asilimia 95 ya watu wawe na uwezo wa kutumia mifumo muhimu ya maji-taka kufikia mwaka 2010.<br>• Kupunguza nusu ya milipuko ya kipindupindu kufikia mwaka 2010.<br>• Kupunguza kiwango cha uchafuzi wa mazingira unaohusiana na maji kutoka asilimia 20 mwaka 2003 hadi asilimia 10 mwaka 2010.<br>• Kupunguza taka hatari za viwandani na kwenye mifereji ya umwagiliaji mashambani.<br>• Kupunguza uwezekano wa kudhurika na majanga ya kimazingira.<br>• Kupunguza uharibifu wa ardhi, misitu na mifumo ya ikolojia ya baharini ambayo watu huitegemea kwa ajili ya uzalishaji mali na kuzaliana.<br>• Kupungua kwa uharibifu wa ardhi na viumbehai. |

**Jedwali Na. 2.4: Mifano ya mikakati ya utekelezaji wa Malengo yanayohusiana na mazingira yaliyopo katika MKUKUTA**

| *Eneo la 1 –Lengo la 2:Kuendeleza ukuaji wa uchumi endelevu* | |
|---|---|
| **Malengo** | **Mikakati** |
| Kupungua athari za mazingira na maisha ya binadamu | kuendeleza shughuli zinazozingatia hatua za usimamizi wa mazingira katika mipango na mikakati. |
| | kubainisha namna ya utekelezaji wa sheria ya usimamizi wa mazingira. |

| | |
|---|---|
| ***Eneo la I –Lengo la 4:Kupunguza umaskini wa kipato miongoni mwa wanaume na wanawake wa vijijini*** | |
| Ongezeko la michango kutoka katika sekta za wanyamapori, misitu, na uvuvi katika kipato cha wakazi wa vijijini. | Kuanzisha programu za kuongeza ushirikishi wa wakazi katika usimamizi wa utunzaji wa maeneo waishio wanyamapori, anzisha mfuko wa wakazi wa usimamizi wa maliasili, kwa kutumia mbinu za asili. |
| | Kuzidisha utunzaji shirikishi wa misitu katika wilaya zote kama njia ya kuziongezea jamii za vijijini kipato kutoka katika mali asili. |
| | Oanisha sera za sekta za maliasili na mikakati; ondoa utata katika sheria na kanuni. Boresha hatua za utunzaji wa ardhi na mbinu shirikishi za usimamizi wa mazingira na ambazo ni rafiki kwa maliasili. |
| ***Eneo la II – Lengo la 3:Ongezeko la uwezo wa watu kupata maji safi, salama na ya gharama nafuu, miundo mbinu bora ya maji- taka, makazi bora, mazingira endelevu na hivyo kupunguza uwezekano wa watu kuathirika na maafa ya kimazingira*** | |
| Kupungua kwa kiwango cha uchafuzi wa mazingira kutoka 20% mwaka 2003 hadi 10% mwaka 2010 | Utekelezaji wa hatua za kupunguza uchafuzi, kuboresha afya na kusimamia viwango vya usalama na utunzaji wa mazingira kama inavyoelekezwa katika sera na sheria za usimamizi wa mazingira. |
| | Utekelezaji wa mkakati wa taifa wa elimu ya mazingira, huku msisitizo ukiwa kuongeza mwamko katika masuala ya afya na maafa ya kimazingira. |
| 100% ya shule ziwe na miundombinu bora ya maji-taka kufikia mwaka 2010 | Hakikisha taasisi za umma kama shule, vituo vya afya, masoko, maeneo ya umma, zina miundo mbinu bora ya maji-taka na kusaidia watu wenye ulemavu kupata huduma zinazotolewa na taasisi hizo. |

| | |
|---|---|
| Kupungua kwa uwezekano wa watu kuathiriwa na majanga ya kimazingira. | Uboreshaji wa usimamizi wa ardhi na matumizi ya tekinolojia za uhifadhi wa vyanzo vya maji, na utekelezaji wa mipango ya taifa iliyo chini ya mikataba ya kimataifa ya mazingira (Multerateral Environmental Agreements-MEAs) ili kuzuia kuenea kwa hali ya jangwa na uharibifu wa ardhi, na kurutubisha ardhi iliyoharibiwa. |
| Uhifadhi wa maliasili na mifumo ya ikolojia ambayo watu huitegemea katika uzalishaji mali.<br><br>Kupungua kwa uharibifu wa ardhi na kutoweka kwa viumbe anuwai | Jenga uwezo wa serikali za mitaa na NEMC kusimamia mifumo asilia ya ikolojia na kulinda rasilimali dhidi ya majanga kwa kutekeleza mipango ya usimamizi wa maliasili. |
| | Utekelezaji wa mbinu na sera ili kuzuia majanga ya kimazingira (mfano: mafuriko, ukame, ongezeko la wakimbizi) na kubainisha mambo ya kufanya majanga hayo yanapotokea. |
| ***Eneo la III – Lengo la 3. Miundo na mifumo ya utawala pamoja na utawala wa sheria ni ya kidemokrasia, shirikishi, wakilishi, inayowajibika na jumuishi.*** | |
| Kuhakikisha uwakilishi, ujumuishaji wa makundi ya watu maskini na walio katika hatari kubwa ya kuathiriwa na majanga na taasisi zinazofanya kazi katika ngazi zote | Kusimamia na shirikisha utekelezaji wa sera na sheria zinazohusika na matumizi na usimamizi wa ardhi na maliasili; ardhi yote ya mijini na vijijini inapimwa na kupewa hati. |
| | Kuimarisha usalama wa umiliki wa ardhi ya vijiji iliyopimwa na inayomikiwa na kijiji, au na mwanakijiji mmoja mmoja na kusimamia kikamilifu maamuzi ya mashauri ya kisheria yanayohusu uchimbaji wa madini, shughuli za umma na uhifadhi wa wanyamapori. |

**Mapungufu ya kujumuisha mazingira katika mipango ya nchi kama inavyojibainisha katika waraka wa MKUKUTA**

Msaada wa kiufundi ili kusaidia uboreshaji wa uingizaji wa masuala ya mazingira katika mipango ya MKUKUTA umefanikiwa sana katika nchi za Tanzania na Msumbiji katika kuendeleza mjadala wa kisera baina ya asasi za kijamii, serikali na washirika wake wa maendeleo, na katika kufasili kiwango cha matokeo ya malengo ya mazingira yaliyopo katika MKUKUTA.

Hata hivyo, nyaraka na michakato hii ya MKUKUTA iliyoboreshwa imekuwa na mafanikio madogo katika upangaji wa bajeti na matumizi halisi ya serikali. Kukosekana huku kwa mafanikio kunaweza kuelezwa kuwa ni udhaifu wa MKUKUTA kama waraka wa kimkakati na mapungufu ya ndani kabisa ya waraka wa mkakati wa kitaifa kama njia ya kupanga matumizi ya rasilimali na vipaumbele.

Uzoefu unabainisha mafunzo makuu matatu:

a) Uhalisia unahitajika kuhusu matokeo yanayotarajiwa kutoakana na ujumuishaji wa mazingira katika MKUKUTA. Hii itasaidia kuinua hadhi ya mazingira katika mijadala ya kisera ya kitaifa, ili kuboresha mitandao mingi zaidi jumuishi kwa ajili ya mijadala ya kisera na kuweka viashiria na malengo yanayofaa. Haitegemewi kuwa na athari katika kiwango cha ugharamiaji kinachotolewa katika shughuli za mazingira au programu nyingine mahsusi zitakazopewa kipaumbele na mashirika yanayoshughulikia mazingira na maliasili.

b) Ili kuleta matokeo katika bajeti na shughuli za sekta ya umma, kujumuisha mazingira unahitaji kutekelezwa ukihusianishwa na sheria na taratibu za kisekta, pamoja na malengo na mamlaka ya asasi.

c) Kubadili kiasi na mwelekeo wa kimkakati wa bajeti za mazingira pia kunaweza kuhitaji umakini wa moja kwa moja wa mashirika yanayojishughulisha na mazingira na maliasili. Hii itahitaji kujumuisha shughuli mbalimbali ili kuongeza kiwango cha upatikanaji wa fedha na hatua za kudhibiti miradi inayofadhiliwa na na kupunguza gharama zisizohitajika na majukumu ya kibajeti. Shughuli hizi zitahitajika kuingizwa katika mikakati ya ngazi zote za serikali na kusimamiwa kupitia mipangilio ya msaada wa bajeti.

## Malengo ya Maendeleo ya Milennia

**Jedwali la 2.5 Mazingira na Malengo ya Maendeleo ya Milenia**

| **Uhusiano wa msingi baina ya mazingira na Malengo ya Maendeleo ya Milenia** | |
|---|---|
| ***Malengo ya Maendeleo ya Milenia*** | ***Mifano ya uhusiano na mazingira*** |
| Kutokomeza umaskini uliokithiri na njaa | Mikakati ya kujiongezea na uhakika wa upatikanaji wa chakula kwa watu maskini mara nyingi hutegemea moja kwa moja mifumo-ikolojia na viumbehai waliotunzwa vizuri. |
| Kutoa elimu ya msingi kwa wote | Muda unaotumiwa na watoto kutafuta maji na kuni unaathiri uwezo wao wa kupata elimu. |
| Kuimarisha harakati za usawa wa kijinsia na kuwawezesha wanawake | Wanawake maskini ndiyo huathiriwa zaidi na uchafuzi wa hewa na mzigo wa kutafuta maji na kuni, na wananyimwa fursa za kumiliki ardhi na maliasili nyinginezo. |
| Kupunguza vifo vya watoto wadogo | Watu takribani milioni 3, wengi wao watoto wadogo chini ya miaka mitano, katika nchi zinazoendelea hufa kila mwaka kutokana na magonjwa kama vile kipindu pindu na kuharisha yanayoenezwa na maji yasiyo salama. |
| Kuboresha afya ya akina mama wajawazito | Uchafuzi wa hewa majumbani na kubeba mizigo mizito huathiri afya ya wanawake na kuwasababishia matatizo wakati wa ujauzito na kujifungua. |
| Kutokomeza magonjwa hatari | 1/5 ya mzigo mkubwa wa magonjwa katika nchi zinazoendelea yanahusishwa na masuala ya mazingira, hivyo hatua za kimazingira za kuzuia magonjwa hayo ni muhimu zaidi ili kupunguza gharama za matibabu ya magionjwa hayo. |
| Kuwezesha mazingira endelevu | Tunapaswa kuzuia ongezeko la uharibifu wa mazingira ili kuboresha afya na uwezo wa mifumo ya ikolojia ya dunia kusaidia uzalishaji mali |

Chanzo: WB (2002) **Kuhusianisha Umaskini na Usimamizi wa Mazingira: Changamoto za Kisera na Mafanikio**

**Maswali ya tathmini:**

**A. Sera za mazingira na mikakati ya kitaifa:**

- Je, Sera ya Mazingira inabainisha wazi malengo ya taifa na mahitaji ya kisheria yanayohusu mazingira?
- Je, kanuni za maendeleo endelevu zinajumuishwa ipasavyo katika Sera?
- Je, malengo ya Sera na mahitaji ya kisheria yako wazi na yanaeleweka?

**B. Ujumuishwaji wa mazingira katika mipango ya taifa**

- Je, malengo ya Sera na mahitaji yanabainishwa katika nyaraka muhimu za mikakati ya kitaifa na kisekta, kama vile mikakati ya kuondoa umasikini na sera za sekta moja moja?
- Je, nyaraka hizi za mikakati zinasaidia katika kupanga mipango na bajeti?

**Marejeo**


Convery, F. J. 1995. Applying Environmental Economics in Africa, World Bank Technical Paper, Number 277

Reed, D (ed). 1992. *Structural Adjustment And the Environment*, Earthscan, London

United Nations. 1992. *Earth Summit Agenda 21: The United Nations Programme of Action From Rio*, United Nations, New York

URT. 2005. *National Strategy for Growth and Reduction of Poverty (NSGRP)* Vice President's Office, Dar es Salaam: Tanzania Printers Ltd.

World Bank. 1991. *Environment and Development in Africa, Selected Case Studies* Economic Development Institute, The World Bank, Washington D. C

World Bank. 1994. *Economy-wide Policies and the Environment, Emerging Lessons From Experience*, The World Bank, Washington D. C

www. Povertymonitoring.go.tz.

# MODULI YA TATU:

## Nadharia ya Mfumo-Ikolojia Katika Uhusiano wa Umaskini na Mazingira

**Malengo ya Moduli**
**Kuhusisha shughuli zinazofanywa katika mifumo-ikolojia na ustawi wa watu**

**Kipindi cha Kwanza**
Katika kipindi hiki, washiriki wanaelekezwa shughuli mbalimbali zinazofanywa katika mifumo-ikolojia na hali ya mawanda mapana ya uhusiano ya umaskini na mazingira. Katika moduli hii pia muundo wa kutathmini shughuli hizo utatolewa. Aidha mambo kadhaa ya ustawi yanayohusiana na shughuli zinazofanywa katika mifumo-ikolojia yatajadiliwa. Moduli hii inalenga kutoa mwanga wa uhusiano mbalimbali yaliyopo baina ya ustawi wa watu – au tuseme kukosekana kwa ustawi wa watu na shughuli zinazofanywa katika mifumo-ikolojia, na baadhi ya mambo yanayobainisha uhusiano huo. Pia mwongozo wenye kanuni muhimu ulioanzishwa na Nobel Laureate Amartya Sen utajadiliwa kama mwongozo ufaao kurejewa katika kupunguza umaskini kwa mtazamo wa mfumo-ikolojia. Mwisho, njia yenye utaratibu ambayo watunga sera wanaweza kuingiza vipengele vya mfumo-ikolojia katika mikakati yao ya kupunguza umaskini itajadiliwa. Tutamaliza moduli hii na maelezo ya jumla ya hoja za msingi zilizojadiliwa na changamoto ambazo serikali mbalimbali zitakabiliana nazo katika suala hili.

Vigezo vitatu vinavyozoeleka ambavyo serikali mbalimbali zitatumia katika kupunguza umaskini kwa kutumia usimamizi endelevu wa mifumo-ikolojia:-

**a)** **Umahsusi** – uhusiano wa umaskini na mazingira lazima uzingatie

hali ya eneo husika. Hali ya eneo husika inahusiana na mifumo mahsusi ya ikolojia na kazi zake kwa wakazi wa maeneo husika, kwa shughuli za kiuchumi, kwa miiko ya kijamii na kiutamaduni, na mwisho, muundo wa kisiasa na kiserikali.

**b)** **Ufasaha** – uhusiano wa umaskini na mfumo wa ikolojia lazima ujadiliwa kwa ufasaha na uwazi hata kama uhusiano huo ni changamani na tata. Lengo ni kwamba tuwe na uwezo wa kutoa mahitimisho ambayo yatawawezesha watunga sera kutunga mikakati itakayoingilia kati. Kwa mfano, kabla hatujatunga mikakati itakayoingilia kati, ni lazima tubaini na kuelewa mambo yanayosababisha uharibifu wa mifumo-ikolojia.

**c)** **Utendaji Kazi** – Mwongozo lazima uwe wa kivitendo zaidi ili watunga sera waweze kuingiza mikakati ya kisera katika mwongozo wa sasa wa kutoa maamuzi kwa urahisi.

**Muda uliopendekezwa**

Muda usiozidi saa tatu kuwasilisha na kujadili mada hii.

**Njia za Ufundishaji**

Mawasilisho/mihadhara, kazi za vikundi, mijadala na mifano mahsusi.

**Malengo**

a) Kubainisha vigezo vinavyoonesha ustawi na viashiria muhimu vya ustawi wa watu vinavyohusiana kwa karibu zaidi na matumizi ya mifumo-ikolojia;

b) Taja aina mbalimbali za shughuli zinazoweza kufanywa kwa kutumia mifumo-ikolojia; na

c) Fafanua uhusiano miongoni mwa mambo mbalimbali yanayoonesha ustawi na viukilio vya ustawi na shughuli mbalimbali ambazo huweza kufanywa kwa kutumia mifumo-ikolojia.

**Utangulizi**

Kufasili shughuli zinazofanywa katika mifumo-ikolojia:-

Shughuli zinazofanywa katika mifumo-ikolojia ni hali na michakato ambayo kwayo mifumo asilia ya ikolojia na spishi mbalimbali ambazo hufanya, huendeleza na husaidia maisha ya binadamu. Huendeleza

viumbe anuwai na uzalishaji wa bidhaa za mifumo-ikolojia kama vile chakula kinachotoka baharini, chakula cha mifugo, mbao, mafuta ya biomasi, nyuzi asilia, madawa na malighafi za viwandani. Zaidi ya kutoa malighafi na huduma, mifumo-ikolojia ni muhimu katika kuwezesha maisha, kama vile kusafisha hewa, maji na udongo pamoja na shughuli za kijamii na kiutamaduni.

**Kisanduku 3.1.**

**Njia endelevu za kujipatia riziki**

Njia za kujipatia riziki hujumuisha uwezo wa kufanya kazi, rasilimali (inajumuisha rasilimali vitu na za kijamii) na shughuli zinazohitajika kufanywa. Njia ya kujipatia riziki inaweza kuonekana endelevu pale inapoweza kuhimili matatizo na kuweza kutunza rasilimali ambazo njia hiyo huzitegemea bila kuathiri vyanzo vya maliasili hizo. Tukichukulia kuwa watu ndiyo kiini cha maendeleo, nadharia ya njia za kujipatia riziki inasisitiza umuhimu wa kuziwezesha sera na mipangilio ya kitaasisi isaidie mahitaji ya jamii maskini. Kwa mfano, kutimiza malengo ya uhifadhi katika eneo fulani mara nyingi kumemaanisha kukomeshwa kwa shughuli za asili ambazo ni muhimu kwa jamii hizi maskini. Hili linaibua matatizo makuu mawili: kwanza, ni dhahiri kwamba jamii maskini zitaathirika pale uhifadhi utakapolazimisha kupunguza kwa matumizi ya mazingira na maliasili zake kwa muda mfupi ili kuyafanya yaweze kuzalisha zaidi baadaye bila ya wao kuwa na mbadala ambao watautumia wakati watakapopunguza kuyatumia hayo. Pili, sera ya namna hiyo haina mashiko katika mtazamo wa kimazingira – kwa mfano, kama watu maskini watazuiwa kukata kuni katika eneo fulani bila ya wao kupewa eneo mbadala, hii itamaanisha kuwafanya wakakate kuni katika misitu mingine ya jirani na hivyo tatizo la uharibifu wa mazingira litakuwa limehamishwa tu kutoka msitu mmoja hadi mwingine. Hivyo suala la “haki za kimazingira” linajaribu kushughulikia suala muhimu la kiasi ambacho kaya, na hasa zinazotegemea sana maliasili kujipatia riziki, zilivyo na uwezo wa

kuzitumia maliasili hizo. Nadharia ya njia endelevu za kujipatia riziki inatilia mkazo ushirikishwaji wa jamii maskini ili kubainisha vikwazo vikuu wanavyokumbana navyo na kutafuta ufumbuzi ulio bora wa matatizo hayo.

**Mambo yanayoonesha ustawi na viukilio vya ustawi vinayohusiana na mifumo-ikolojia**

Mwezeshaji abainishe yafuatayo:

Watu wote – maskini na matajiri; waishio katika nchi zinazoendelea au zilizoendelea- wanategemea kupata ustawi kutokana shughuli zinazofanywa katika mifumo ya ikolojia. Hata hivyo, bainisha kwamba uteuzi wa mwisho wa mambo yanayoonesha ustawi na uhusiano wake na shughuli zifanywazo katika mifumo ya ikolojia vinapaswa kubainishwa na jamii au watu husika, kinadharia kupitia ushirikishwaji wa jamii hizo.

**Kisanduku cha 3.2**

**Baadhi ya mambo muhimu yanayoonesha ustawi ambayo yanapaswa kusisitizwa ni yafuatayo:-**

- Kuwa na uwezo wa kujipatia chakula.
- Kuepukana na magonjwa yanayoweza kuzuilika.
- Kuishi katika mazingira safi na salama.
- Kupata maji safi na salama.
- Kupata hewa safi.
- Kupata nishati kwa ajili ya kupikia na kujipatia joto.
- Kutumia tiba zao za asili.
- Kuendelea kutumia vitu vya asili vinavyopatikana katika mifumo ya ikolojia kwa ajili ya shughuli zao za kitamaduni na kidini.
- Kukabiliana na majanga makubwa ya asili kama vile mafuriko, tufani na maporomoko ya ardhi.
- Kutoa mamuzi endelevu ya kiutawala yanayojali maliasili na kuwezesha mkondo wa upatikanaji wa kipato endelevu

Mwezeshaji abainishe kwamba mambo 10 katika Kisanduku 3.2 ni maelezo ya kina ya uainishaji mpana ya Benki ya Dunia katika masuala ya afya na uwezekano wa kuathiriwa na njia za kujipatia riziki. Inaonesha maendeleo yanaweza pia kutazamwa kama ufafanuzi mkubwa zaidi wa uainishaji mpana wa afya, uwezekano wa kuathiriwa na njia za kujipatia riziki. Benki ya Dunia hutumia maelezo haya katika nadharia yake ya kuonesha uhusiano baina ya umaskini na mazingira. Vinafanana na dhana za dhima na uwezo, ambazo Amartya Sen anadai kwamba ni muhimu kwa kutathmini ustawi wa watu.

Mwezeshaji asisitize kwamba kutia mkazo kwenye uwezo wa watendaji, tunaweza pia kupanua nafasi ya taarifa katika kutathmini na kupima ufahamu na utekelezaji wa sera katika kuleta ustawi na kupunguza umaskini. Shughuli mbalimbali zinazofanywa katika mifumo-ikolojia zinaweza kugawanywa katika makundi makuu matatu kama ifuatavyo:-

a) Utoaji;
b) Urekebishaji; na
c) Kutajirisha/kiutamaduni.

**Shughuli zinazofanywa katika mifumo-ikolojia**

**Shughuli za utoaji**

Hii inahusu maliasili ambazo kimsingi hutumika kwa ajili ya shughuli za kiuchumi. Kiwango cha mchango wake katika ustawi kwa kawaida hupimwa kwa kiwango cha bidhaa kilichopatikana kutoka katika maliasili hizo. Baadhi ya vitu vinavyotolewa na mifumo-ikolojia katika mchakato mzima wa kutafuta ustawi inajumuisha vitu vifuatavyo:-

a) Chakula;
b) Mazao ya viumbe hai, mimea na wanyama;
c) Vitu vya kinasaba, kemikali asilia na madawa;
d) Mafuta/nishati;
e) Nyuzi;
f) Viumbe visivyo na uhai; na
g) Maji safi.

**Shughuli urekebishaji**

**Shughuli hizi** wakati mwingine huitwa "usaidiaji", kama dhima ya moja kwa moja ambayo mifumo ya ikolojia huifanya katika kusaidia binadamu waishio humo kuweza kuishi. Hizi ni dhima ambazo mara nyingi husahauliwa na jamii. Dhima za urekebishaji zinazofanywa na mifumo ya ikolojia na kuchangia katika ustawi zinajumuisha yafuatayo:-

a) Kusafisha maji na hewa;
b) Uzuiaji wa mafuriko na ukame;
c) Upunguzaji wa sumu na kusaidia umeng'enyaji wa taka;
d) Kurejesha rutuba ya ardhi;
e) Uchavushaji wa mazao na mimea asili;
f) Udhibiti wa wadudu waharibifu wa mazao;
g) Utawanyaji wa mbegu na usambazaji wa virutubisho vya mimea;
h) Uhifadhi wa viumbe anuwai, ambao kwao binadamu hunufaika kwa kilimo, madawa na malighafi za viwandani;
i) Ukingaji dhidi ya mionzi hatari itokayo kwenye jua;
j) Uhifadhi wa hali ya hewa, upunguzaji wa joto, mwendokasi wa pepo na mawimbi.

**Shughuli za kiutamaduni**

Shughuli hizi, au shughuli za kujitajirisha ni miongoni mwa shughuli zifanywazo katika mifumo ya ikolojia ambazo husahauliwa sana, na hasa katika nchi zilinazoendelea. Dini na tamaduni nyingi zinaamini kwamba viumbe asili ni kitu kinachoishi na hivyo waumini wengi wa dini na tamaduni hizo huomba viumbe asili mbalimbali.

Shughuli za kiutamaduni au za kutajirisha zinazofanywa katika mifumo-ikolojia zinajumuisha yafuatayo:-

a) Shughuli za kiimani na mahusiano ya watu na ardhi na maji;
b) Mambo ya umbuji;
c) Mahusiano ya kijamii na mila; na mambo ya kitaaluma na kisayansi.

## Kipindi cha Pili

### Hali ya ustawi wa watu

Mwezeshaji abainishe kwamba ustawi wa watu ni tata na una mambo mengi na viukilio vinavyotegemea sana hali ya shughuli zinazofanywa katika mifumo ya ikolojia; pia kwamba, ni vipengele na viukilio vile tu vya ustawi viavyoathiriwa moja kwa moja na hali ya shughuli zinazofanywa katika mifumo ya ikolojia zinajadiliwa katika moduli hii.

Ongezeko kubwa la idadi ya watu pekee haliwezi kusababisha uharibifu wa mazingira. Kuna ushahidi halisi kwamba baadhi ya kaya na jamii za wakulima zimegundua tekinolojia na taasisi za usimamizi/uhifadhi wa mazingira kutokana na ongezeko la kupungua kwa rasilimali. Ingawaje, ugunduzi kama huo hautokei katika maeneo yote, na hivyo kuna haja ya kuungwa mkono na kusaidiwa kwa mikakati ya kisera na uingiliaji kati mwingine (kwa mfano, katika maeneo ya umiliki, mafunzo ya utafiti wa kilimo, n.k.). Maeneo yanayopaswa kupewa kipaumbele katika uingiliaji kati huo ni yale yaliyo madogo lakini yenye idadi kubwa ya watu.

Uharibifu wa mazingira unaweza kuchangia ongezeko kubwa zaidi la idadi ya watu kwa kuongeza hitaji la nguvu katika familia (kwa mfano, haja ya kuzidi kwenda mbali na nyumbani kutafuta malisho ya mifugo, kuchota maji na kukusanya kuni, n.k.). Kinyume chake, uboreshaji wa usimamizi wa mazingira unaopunguza uharibifu wa mazingira unaweza kutafsiriwa kuwa kupungua kwa mahitaji ya nguvu kazi humaanisha kupungua kwa kuzaliana kwa watu.

**Jedwali la 3.1: Mambo yanayoashiria ustawi wa jamii yenye matatizo kimikoa**

| Mkoa | Mambo yanayoashiria ustawi yenye matatizo | Mkoa | Mambo yanayoashiria ustawi yenye matatizo |
|---|---|---|---|
| Arusha | Chakula cha kutosha | Morogoro | Chakula cha kutosha |
| 1.1.1 | Maji safi na salama ya kutosha | 1.1.2 | Maji safi na salama ya kutosha |
| 1.1.3 | Nishati | 1.1.4 | Nishati |
| 1.1.5 | Uwezo wa kuishi. | 1.1.6 | Uwezo wa kuishi. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Dar es Salaam | Maji safi na salama ya kutosha | Mtwara | Maji safi na salama ya kutosha |
| 1.1.7 | Uwezo wa kuishi | 1.1.8 | Uwezo wa kuishi |
| Dodoma | Chakula cha kutosha | Mwanza | Maji safi na salama ya kutosha |
| 1.1.9 | Maji safi na salama ya kutosha | P e m b a North | Maji safi na salama ya kutosha |
| 1.1.10 | Nishati | 1.1.11 | Uwezo wa kuishi |
| 1.1.12 | Uwezo wa kuishi. | P e m b a South | Maji safi na salama ya kutosha |
| Iringa | Maji safi na salama ya kutosha | 1.1.13 | Uwezo wa kuishi |
| 1.1.14 | Uwezo wa kuishi | Pwani | Chakula cha kutosha |
| Kagera | Maji safi na salama ya kutosha | 1.1.15 | Maji safi na salama ya kutosha |
| 1.1.16 | Nishati | 1.1.17 | Nishati |
| 1.1.18 | Uwezo wa kushi | 1.1.19 | Uwezo wa kuishi. |
| Kigoma | Maji safi na salama ya kutosha | Rukwa | Maji safi na salama ya kutosha |
| 1.1.20 | Nishati | 1.1.21 | Uwezo wa kuishi |
| 1.1.22 | Uwezo wa kuishi | Ruvuma | Maji safi na salama ya kutosha |
| Kilimanjaro | Chakula cha kutosha | 1.1.23 | Uwezo wa kuishi |
| 1.1.24 | Maji safi na salama ya kutosha | Shinyanga | Chakula cha kutosha |
| 1.1.25 | Nishati | 1.1.26 | Maji safi na salama ya kutosha |
| 1.1.27 | Kipato cha kutosha | 1.1.28 | Nishati |
| Lindi | Chakula cha kutosha | 1.1.29 | Uwezo wa kuishi. |
| 1.1.30 | Maji safi na salama ya kutosha | Singida | Chakula cha kutosha |
| 1.1.31 | Nishati | 1.1.32 | Maji safi na salama ya kutosha |
| 1.1.33 | Kipato cha kutosha. | 1.1.34 | Nishati |
| Manyara | Chakula cha kutosha | 1.1.35 | Uwezo wa kuishi. |
| 1.1.36 | Maji safi na salama ya kutosha | Tabora | Chakula cha kutosha |
| 1.1.37 | Chakula cha kutosha. | 1.1.38 | Maji safi na salama ya kutosha |
| Mara | Chakula cha kutosha | 1.1.39 | Uwezo wa kuishi |
| 1.1.40 | 1.1.41 | Tanga | Chakula cha kutosha |
| 1.1.42 | 1.1.43 | 1.1.44 | Maji safi na salama ya kutosha |
| Mbeya | Maji safi na salama ya kutosha | 1.1.45 | Uwezo wa kuishi |
| 1.1.46 | Chakula cha kutosha. | **1.1.47** | **1.1.48** |

Kuna mambo mengi yanayoleteleza uhusiano mbaya baina ya ustawi na mifumo-ikolojia. Baadhi ya mambo hayo ni:-

a) Kushindwa kitaasisi;
b) Ukosefu wa mbinu zifaazo;
c) Mashirika ya serikali yasiyofanya kazi kwa ufanisi;
d) Kutoshirikishwa na kutokuhusishwa kwa watu maskini katika kufanya maamuzi;
e) Ukosefu wa miundombinu ya kiuchumi;
f) Ukosefu wa mianya ya kijamii kama vile mitandao ya usalama;
g) Ukandamizaji wa kijinsia;
h) Ukosefu wa usalama wa mifumo ya ikolojia, kwa maana ya ukosefu wa ulinzi wa mifumo ya ikolojia dhidi ya majanga; na
i) Urasimu na kutowajibika kwa taasisi rasmi kunakosababishwa na kukosekana kwa uwazi katika umiliki wa rasilimali muhimu na kutozingatiwa kwa haki katika zoezi zima la ubinafsishaji wa rasilimali hizo.

**Mchoro wa 3.1: Hatua za tathmini ya mifumo ya ikoloji**



**Maswali ya mapitio**

- Je, ni shughuli gani za kiikolojia ambazo Tanzania haiwezi kuishi bila hizo kuwepo?
- Je, ni mifumo gani ya ikolojia ambapo shughuli hizo hufanyika?
- Mifumo hiyo ya ikolojia ina hadhi na mwelekeo gani?

**Marejeo**

Hassan, R. M (ed.). *Accounting for Stock and Flow Values of Woody Land Resources: Methods and Results from South Africa*, Centre for Environmental Economics and Policy in Africa, Pretoria.

Turton, A na R. Henwood (eds.) 2002. *Hydropolitics in the Developing World, A Southern Africa Perspective,* Africa Walter Issues Research Unit, Pretoria

United Nations. 1992. *Earth Summit Agenda 21: The United Nations Programme of Action From Rio*, United Nations, New York

# MODULI YA NNE:

## Kugharamia Uhifadhi wa Mazingira

**Malengo ya Moduli**

Katika moduli hii washiriki wataelekezwa masuala mbalimbali yanayohusu kupanga bajeti ya kugharamia utunzaji wa mazingira. Uelewa mzuri wa matumizi ya fedha za umma katika uhifadhi wa mazingira ndicho kipimo kizuri cha ubora na ufanisi wa usimamizi wa fedha za mazingira. Moduli hii itasaidia kuibua mwamko wa usimamizi bora wa fedha za uhifadhi wa mazingira kwa ujumla. Vyanzo mbalimbali vya mapato ya fedha za kuhifadhi mazingira vitajadiliwa katika moduli hii, kwa mfano kodi, ada, ushuru, tozo, n.k. Ni vema kuangalia umuhimu wa mageuzi katika hazina ya mazingira ambayo yataanzisha kodi za mazingira, ushuru wa watumiaji wa mazingira, ushuru kwa wachafuzi wa mazingira, vibali vinavyoonesha viwango vya utupaji taka kwenye mazingira na mengineyo. Moduli hii pia inabainisha mchango wa washirika wa maendeleo unavyoweza kusaidia juhudi za kuhifadhi mazingira kwa maana ya kuisaidia bajeti ya uhifadhi wa mazingira na mengineyo. Mambo hayo ni pamoja na kuongeza bajeti ya mazingira na inayoweza kutumika kuendeleza uhifadhi wa mazingira na kuchangia katika kupunguza umaskini.

**Muda uliopendekezwa**

Tumia muda usiozidi saa tatu kuwasilisha na kujadili kipengele hiki. Muda huu unaweza kugawanywa katika mawasilisho na kazi za vikundi kama itakavyohitaji, kutegemeana na mbinu ya ufundishaji. _

**Shughuli na majukumu ya kufanya**

Mchanganyiko wa mbinu za ufundishaji unaojumuisha mawasilisho, kazi za vikundi, mijadala na mifano mahsusi ndiyo unaopendekezwa hapa. Mbinu hii ni ili kuruhusu ushirikishwaji na mwingiliano miongoni mwa wanafunzi.

**Malengo**

Moduli hii inakusudia:

a) Kubainisha maeneo muhimu ya kugharamia mazingira kwa ajili ya kupunguza umaskini;

b) Kuonesha mchango wa rasilimali za mazingira katika pato la taifa ;

c) Kuvielezea vyanzo vingine mbalimbali ambavyo vinaweza kutumika kugharamia mazingira.

d) Moduli hii pia inatoa taarifa na mwongozo katika mambo yafuatayo:

   i) Changamoto katika kufasiri vipaumbele na mipango ya mazingira katika kupanga bajeti na matumizi ya umma.

   ii) Mchango wa makundi mbalimbali yanayoendeleza juhudi za uhifadhi wa mazingira katika kuendeleza vipaumbele vya mazingira, kushawishi kuongezwa kwa bajeti ya mazingira na kusimamia bajeti za mazingira zilizowekwa, na matokeo yake.

e) Matumizi ya mbinu nyingine za misaada katika kusaidia malengo ya mazingira na kuwezesha kuingizwa kwa malengo hayo katika mipango ya kusaidia bajeti.

Mwezeshaji aanze kwa kutoa maelezo ya jumla ya ugharamiaji wa umma katika programu za mazingira kuhusu mifuko ya mazingira.

## MIFUKO YA MAZINGIRA

Kipengele hiki kinaweza kuanza kwa kutoa maelezo ya jumla ya mifuko ya mazingira.

- Jadili na changia mawazo juu ya nini hasa maana ya mifuko ya mazingira.

**Kisanduku 4.1**

**Baadhi ya mambo ya msingi juu ya mifuko ya mazingira ni kama ifuatavyo:**

- Mifuko ya mazingira ni taasisi ambazo zimeanzishwa ili kuelekeza fedha zinazotolewa kwa ajili ya uhifadhi wa mazingira katika matumizi yaliyokusudiwa ya utunzaji na uendelezaji wa mazingira na si katika matumizi mengine ya serikali.
- Mifuko ya mazingira hutumia mapato yake yaliyotengwa kusaidia miradi mbalimbali ya uhifadhi wa mazingira.
- Mifuko ya mazingira ipo katika nchi zilizoendelea na hata zinazoendelea ila inatofautiana kutokana na kiwango cha maendeleo ya kiuchumi ya nchi husika.
- Mifuko ya mazingira iliyopo katika nchi zilizoendelea hushughulikia tatizo maalum wakati ile iliyopo katika nchi zinazoendelea ina malengo ya kiujumla.
- Katika nchi zinazoendelea ambazo zinajaribu kupunguza mchango wa serikali katika uhifadhi wa mazingira na zinazojaribu kupata maendeleo ya kibiashara, utegemezi huwa katika wagharimiaji binafsi wa miradi ya uhifadhi wa mazingira; hivyo nyingi hutumia kanuni ya "wachafuzi wa mazingira kugharamia usafishaji wa mazingira".

### Vyanzo vya fedha vya mifuko ya mazingira

Jadili baadhi ya vyanzo muhimu vya fedha vya mifuko hii. Baadhi ya vyanzo hivyo ni kanuni ya mchafuzi wa mazingira kulipa. Hii ina maana kwamba mchafuzi wa mazingira anapaswa kubeba mzigo wa gharama ya kuyarekebisha mazingira ili yafikie viwango vinavyohitajika.

- Gharama za kufikia viwango hivyo itategemea faida ya kiwanda/mradi unaochafua mazingira, kuongezwa kwa usawa au kutoka katika mikopo.
- Msaada wa kifedha uliotolewa na serikali. Katika kanuni hii, msaada

utatolewa katika masuala maalumu mfano:

- pale ambapo msaada huu usipotolewa utaathiri biashara ya nje na kiwango cha uwekezaji.
- pale ambapo sekta fulani za kiuchumi au za viwanda zitapata matatizo makubwa zisipopata msaada huo. Msaada huo hata hivyo utatolewa kwa muda maalum utakaokubaliwa, na utalenga kutatua matatizo ya kiuchumi yenye mwelekeo wa kijamii ambao umetokana na sera za mazingira.

**Kisanduku 4.2 Kanuni ya Mchafuzi Kugharamia**

Kanuni hii, kwa hiyo, inaeleza kwamba mchafuzi wa mazingira atabeba gharama za kupunguza uchafuzi anaousababisha katika mazingira, wakati mchango wa serikali utatolewa katika kugharamia rasilimali za umma kama vile: kutunza asili na viumbe anuwai, usimamizi wa mazingira, na tafiti na kukuza mwamko wa umma.

Jadili baadhi ya changamoto za kutumia kanuni hii, yaani kanuni ya mchafuzi wa mazingira kugharamia uhifadhi wa mazingira, na kuendeleza mfumo bora wa uhifadhi wa mazingira.

**Kisanduku 4.3 Changamoto za Utekelezaji wa Kanuni**

Baadhi ya changamoto ni kama ifuatavyo:

- Udhaifu unaotokana na uwezo mdogo wa kutekeleza mikakati ya uhifadhi wa mazingira.
- Matatizo makubwa ya kiuchumi ya viwanda/mradi husika, na hivyo kuzuia uwezo wa kuibadili rasilimali inayochafua na isiyochafua mazingira.
- Ugumu katika kubadili sera za kifedha ili kuongeza kipato cha taifa na manispaa kugharamia za utunzaji wa mazingira.
- Kutokukamilika kwa zoezi la ubinafsishaji na hivyo kuzuia mabadiliko muhimu ya kiusimamizi katika viwanda/mashirika mbalimbali.

- Ushirikishwaji mdogo wa sekta ya benki katika kugharamia miradi ya utunzaji wa mazingira
- Kutokukomaa kwa mtaji ambao ungesaidia kugharamia mradi.
- Ukosefu wa taarifa sahihi juu ya uharibifu wa mazingira na athari zake katika jamii.
- Mifuko ya mazingira inawakilisha dhana inayosaidia kutatua matatizo hayo katika uchumi unaoendelea. Zaidi ya kutoa msaada wa kifedha na ruzuku kwa mashirika yanayotunza mazingira, inaweza kushirikiana na taasisi za kifedha ili kuhamisha wataalamu wanaohitajika katika sekta binafsi.

Msisitizo juu ya ufanisi wa Sera za mazingira, mifuko ya mazingira inaweza kuelekeza fedha kwenye matatizo makubwa ya kimazingira yanayoiathiri jamii na kuhakikisha matumizi bora.

Kwa upande mwingine, ruzuku yoyote kwenye kiwango cha biashara cha riba katika mikopo kinawakilisha fedha itakayoimarisha sera nyingine za mazingira ili kulinda kiwango cha ubora wa mazingira na hatua nyingine za kiuchumi.

a) Onesha kwamba vyanzo vingine vya mapato ya mifuko ya mazingira vinatoka katika ada za mazingira, faini na kodi, misaada ya kimataifa na ya ndani, kama nyongeza ya bajeti ya taifa.

b) Mifano ya ada za mazingira ni ada za kuingia kwenye maeneo ya hifadhi, tozo kwa malighafi zinazozalisha bidhaa, n.k, zinazochafua mazingira.

c) Sisitiza kwamba, ni muhimu kuwa na msingi wa kisheria ili kuhakikisha uwezekano wa kuanzisha ada, zaidi ya kuwepo kwa usimamizi mzuri wa ukusanyaji wa ada hizo.

d) Bainisha kwamba mifuko mizuri zaidi ya mazingira ni ile ambayo imepangwa vizuri na inafanya kazi vizuri.

**Kisanduku 4.4 Vigezo vya Mifuko ya Mazingira**
**Baadhi ya vigezo hivyo ni kama:**

- Kuepuka au kupunguza tatizo la muda mrefu la kukosekana kwa ufanisi katika usimamizi wa fedha. Matumizi yanapaswa kuelekezwa katika vipaumbele na miradi ya mazingira yenye faida kubwa ukilinganisha na gharama zake.
- Mifuko ya mazingira inapaswa kufanya kazi ya kuchangia na kusaidia uboreshaji wa mazingira, na si kuwa na ushindani wa kimtaji.
- Mifuko ya mazingira inapaswa kusaidia mbinu na mikakati mingine ya kisera katika uhifadhi wa mazingira.
- Mifuko ya mazingira inapaswa kuwa na mkakati wa kiujumla wa kutoa fedha za kugharamia mazingira, kufuata njia zilizo wazi katika kuteua miradi ya kuigharamia ili kuhakikisha kuwa fedha zinazotolewa zinatumika vizuri. Utaratibu mzuri wa usimamizi na kutathmini shughuli za uhifadhi wa mazingira, na kutumia vizuri wataalamu wa ndani na wa nje katika kuhakikisha kunakuwa na ufanisi katika utawala.
- Mifuko ya mazingira inapaswa kukuza ongezeko la rasilimali za sekta binafsi na utoaji wa mitaji kwa ajili ya miradi ya utunzaji wa mazingira.
- Katika kuanzisha na kutathmini vyanzo vya mapato vya mifuko ya mazingira, mamlaka za mazingira zinapaswa kuhakiki ufanisi wake katika utunzaji wa mazingira, kiuchumi na kiutawala, usawa na kukubalika kwake kwa jamii husika.
- Mifuko ya mazingira inapaswa kuwa na uwazi na inapaswa kuwajibika kwa matendo yao kwa serikali, mabunge, na umma wote.

Kila mfuko wa mazingira una utawala ambao upo katika mfumo wa bodi ya wakurugenzi au kamati ya usimamizi ambayo inaendesha shughuli zake, kupanga mikakati yake, kutoa maamuzi na kusimamia utekelezaji wake.

Kwa hiyo, ugharimiaji wa miradi unatumia programu ya ushindani ya miradi (CPP) ambayo inatekelezwa kwa kutumia mzunguko wa mradi

unaojumuisha shughuli zifuatazo:-

a) Kupanga vipaumbele vya mazingira kwa ajili ya miradi. Kwa kawaida hii hutegemea mipango ya mazingira ya nchi au mamlaka za kikanda n.k.

b) Kutafsiri vipaumbele katika kutathmini na vigezo vya kuteua mradi toka katika miradi inayoomba fedha. Vigezo vilivyoteuliwa vinachapishwa ili kuruhusu haki na usawa katika kuomba msaada.

c) Kutathmini na kuteua miradi itakayosaidiwa kwa mujibu wa vigezo vilivyowekwa..

d) Kukubaliana masharti na maelezo ya miradi itakayopokea msaada na kukamilisha makubaliano mbalimbali ya kifedha na kisheria, ikiwemo kutoa fedha na kutoa masharti husika, kusimamia na kuangalia mahitaji na kukamilisha makubaliano yote ya kibenki pale yanapohitajika.

e) Kutathmini namna ya kutoa fedha kama msaada, mkopo wa moja kwa moja, ruzuku ya riba ya mkopo wa kibiashara, kutoa dhamana ya mkopo/mikopo kupitia taasisi za fedha au uwekezaji wa moja kwa moja.

f) Kusimamia, kutathmini, na ulipaji kwa kila mradi, iwe moja kwa moja au si moja kwa moja kupitia washauri wanaotambuliwa. Mifuko ya mazingira inapaswa kufanya kazi ya kuhakikisha ina vyanzo vyake vya kipato ambavyo kwavyo ada ya mazingira inachukua nafasi kubwa.

***Maendeleo ya kitaasisi na kiuwezo***

a) Onesha uhusiano wa umaskini na mazingira katika mipango ya serikali: jenga mbinu ya muda mrefu ya kuingiza mazingira kwenye mipango ya kisekta ili kuhakikisha uingizwaji wa masuala yahusuyo umaskini na mazingira katika mipango ya maendeleo, bajeti, programu za sekta na utekelezaji wake. Sisitiza umuhimu wa kuingiza umaskini na mazingira katika njia na mifumo ya utawala ya mashirika husika.

b) Kuandaa mkakati wa kujenga uwezo: onesha umuhimu wa kuweka mkakati ulio wazi wa kujenga uwezo unaoshughulikia mahitaji ya kiuwezo ya muda mrefu kwa ajili ya tathmini na uchambuzi,

uingizaji wa mazingira katika mchakato wa sera, uingiliano katika sera na kuendeleza programu, kupanga bajeti, kutoa fedha, utekelezaji na usimamizi wake. Hivyo ni muhimu kuendelea kujenga mahitaji na uwezo wa taasisi kwa kuendeleza maeendeleo ya kiuwezo uliopatikana katika awamu zilizopita.

c) Kuandaa mkakati wa kujenga uwezo kwa vitendo: Mkakati huu utegemee mahitaji ya watendaji mbalimbali wa serikali na wadau wengine. Andaa warsha, mafunzo kazini, shirikisha wadau wengine kujadili juu ya shughuli bora za kuhifadhi mazingira na kuondoa umaskini kwa kutoa mifano mahsusi, na mbinu nyingine.

**Msaada wa Ujumla kupitia Bajeti**

Msaada wa Ujumla katika bajeti ni namna mpya ya msaada. Tabia zake kuu zinajumuisha utoaji wa pamoja wa rasilimali za bajeti zisizofungwa; msisitizo ukiwa katika mchakato wa kisera nchini (mfano, mikakati ya kupunguza umaskini); mkazo pia unapaswa kuwekwa katika malengo ya maendeleo ya taasisi (kama vile kuboresha upangaji na uwezo wa usimamizi wa fedha); na matumizi ya njia zinazotabirika na zilizo wazi kwa misaada ya nje, inayofanya kazi kupitia mifumo ya serikali.

Hii ni njia ya kutoa fedha kupitia bajeti ya serikali, ni mkakati wa kisera uliopitishwa. Si njia ya kulazimisha mabadiliko ya sera pale msaada wa ndani wa mabadiliko unapokosekana.

a) Msaada wa Ujumla katika bajeti (GBS) unaonekana kama mbinu ya kimsaada ambayo kwa kiasi kikubwa unaendana na sera na mifumo ya kitaifa.

b) Kuongezeka kwa matumizi yake kunaleta matumaini ya kuondoa, kwa njia ya ubunifu wa namna yake, tatizo la ukosefu wa fedha za kugharamia malengo ya mazingira.

c) Msaada katika bajeti unaweza kutoa nyongeza madhubuti na utoaji wa fedha wenye uwezo mkubwa wa kubadilika badilika katika bajeti za sekta za umma, kupitia njia ambayo inagharama ndogo, inayofanya kazi ya kuimarisha usimamizi wa taifa wa fedha na mifumo ya uwajibikaji, na kuipa nchi husika uwezo mkubwa wa kusimamia matumizi ya rasilimali.

d) Udhibiti huu unafanywa kupitia taasisi za kidemokrasia; kwa kawaida ndizo husimamia michakato ya bajeti, na hivyo kusaidia maendeleo ya nchi husika.

e) Pia msisitizo kwamba, muundo wa usimamizi utumikao mara nyingi kwa ajili ya Msaada wa Ujumla wa bajeti unatoa mbinu muhimu ya kuwa na mjadala wa kimkakati baina ya serikali na washirika wa maendeleo kuhusu sera na michakato ya kimageuzi inayopaswa kupewa kipaumbele.

f) Hili linatoa matumaini ya kuweka sera ya mazingira na usimamizi endelevu wa maliasili imara zaidi miongoni mwa vipaumbele vya sera za nchi zinazoendelea zinazopokea msaada wa bajeti (GBS).

g) Matumizi ya msaada katika bajeti unatoa mianya kadhaa ya kusaidia miradi ya taifa ya mazingira.

   i) Kwanza, inatoa matumaini ya kuongezeka fedha zitakazotolewa kupitia bajeti (inapunguza mzigo wa gharama kwa mashirika mengine yanayoshughulikia mazingira).

   ii) Pili, inaweza kuimarisha michakato ya bajeti katika wizara ya mazingira na kuongeza umiliki wa mipango ya matumizi ya mazingira.

   iii) Tatu, inatoa matumaini ya mabadiliko mapana ya mfumo kupitia mawasiliano na wizara ya fedha na serikali kwa ujumla (mfano, kuharakisha mageuzi ya muundo wa udhibiti na kuanzisha mchujo ulio wazi wa mazingira).

   iv) Nne, inaimarisha mchango wa makundi mengine yanayoshugulika na mazingira (SWGs) katika kusaidia mijadala ya sera za mbalimbali.

   v) Na mwisho, inatoa nafasi ya kutoa maamuzi yahusuyo mazingira kwa njia iliyo na uwazi zaidi (mfano, kutegemeana na uchunguzi wa Bunge).

**Nafasi ya Msaada wa Ujumla kupitia bajeti kwa sekta ya mazingira**

Utoaji wa Msaada wa Ujumla katika bajeti unaweza kuleta manufaa kwenye sekta ya mazingira katika maeneo makuu matatu:-

a) Kwa kuongeza fedha katika bajeti, kunawezesha mashirika mengine

ya mazingira kupata msaada wa nyongeza kutoka katika bajeti na pia inasaidia wizara ya mazingira kutekeleza mipango ya bajeti ihusuyo mazingira kama ilivyokuwa imepangwa.

b) Kwa kuweka umuhimu mkubwa katika bajeti ya taifa na kuimarisha mifumo ya taifa ya usimamizi wa fedha za umma, inaweza kuimarisha moja kwa moja uwazi na uwajibikaji katika bajeti ya sekta ya mazingira na pia inaweza kuwavutia washirika wa maendeleo kuchangia bajeti na kuanzisha miradi ya mazingira na hivyo kuimarisha mambo mengine hata kama si moja kwa moja.

c) Mwisho, kwa kuleta aina nyingine ya majadiliano, inaweza kusaidia kupata ufumbuzi wa masuala ya muda mrefu ya sera na/au kuharakisha utekelezaji wa mageuzi ya sasa ya sera.

**Kisanduku 4.5 Changamoto za Mikakati ya Kupunguza Umaskini**

**1.1.52**

**Tambua matatizo ya harakati za uhifadhi wa mazingira kupitia mikakati ya kupunguza umaskini (PRS)**

Msaada wa kiufundi kusaidia harakati za kuboresha mazingira katika mikakati ya kupunguza umaskini (PRS) umefanikiwa sana Tanzania na Mozambique katika kuimarisha mjadala wa kitaifa na kuinua mwamko wa umma katika masuala ya mazingira, katika kuunda mitandao ya mijadala ya kisera miongoni mwa taasisi za kijamii, serikali na washirika wake wa maendeleo, na katika kufasili kiwango-mkakati cha matokeo ya malengo ya kimazingira yaliyoingizwa katika mikakati ya kupunguza umaskini.

1.1.53

Lakini, pamoja na jitihada hizi za kuboresha nyaraka za mikakati ya kupunguza umaskini na michakato haijawa na mchango mkubwa katika upangaji wa bajeti na programu halisi za matumizi ya fedha. Upungufu hu unaweza kuelezwa kwamba ni udhaifu wa programu za mikakati ya kupunguza umaskini (PRSP) kama nyaraka za kimkakati, na upungufu wa ndani wa nyaraka za mikakati ya kitaifa

kama kifaa cha kugawa na kutoa kipaumbele cha rasilimali.

1.1.54
Uzoefu unatufundish mambo makuu matatu:-

a) Uhalisia unahitajika kutokana na athari inayoweza kutokea ya harakati kubwa za uhifadhi wa mazingira katika mikakati ya kupunguza umaskini. Unaweza kusaidia kupandisha hadhi ya mazingira katika mjadala ya sera ya taifa ili kusaidia mitandao jumuishi zaidi ya mjadala wa sera ya taifa na kuweka viukilio na malengo ya kiwango kinachostahili. Hata hivyo haitarajiwi kuwa na athari kubwa katika kiwango cha utoaji wa fedha kwa ajili ya shughuli za utunzaji wa mazingira au kwa programu maalum ambayo itapewa kipaumbele na mashirika ya utunzaji wa mazingira na ya uhifadhi wa maliasili.
b) Ili kuleta manufaa katika bajeti na shughuli za sekta za umma, harakati za utunzaji wa mazingira zinahitaji kufanywa kwa kuhusishwa na sheria na taratibu za sekta ya mazingira; pia na malengo na mamlaka ya mashirika husika.
c) Kubadilisha ukubwa na mwelekeo wa bajeti za mazingira pia kunaweza kuhitaji umakini wa moja kwa moja wa mashirika yanayojishughulisha na uhifadhi wa mazingira. Hili litahitaji kuunganisha shughuli ili kuongeza upatikanaji wa fedha na hatua za udhibiti wa miradi inayopata fedha toka nje na kupunguza gharama na majukumu ya kibajeti yasiyohitajika. Shughuli hizi zinahitaji kuingizwa katika mikakati ya kitaifa yenye masharti ya kati, na kusimamiwa kupitia mipangilio ya msaada katika bajeti.

**Matumizi ya kodi za mazingira na ada za watumiaji (mageuzi ya hazina ya mazingira)**

a) Msisitizo ni kwamba mkakati huu muhimu unatumia fedha za ndani ya nchi k.v. kodi, tozo na ada.
b) Pia, hiki ni chanzo cha fedha ambacho kinafanya kazi kwa kiasi kikubwa sambamba na mchakato wa bajeti ya serikali wenye taarifa za ukusanyaji wa mapato na matumizi yake.

**Kudhibiti matumizi ya kodi za mazingira na ada za watumiaji kugharamia moja kwa moja mashirika yanayoshughulikia utunzaji wa mazingira**

Hiki ni chanzo muhimu cha fedha za kugharamia mashirika yanayojishughulisha na utunzaji wa mazingira na maliasili, hasa Tanzania. Pia nchi nyingine za Afrika zina mkakati kama huu, kwa mfano, Ghana na Msumbiji.

Mkakati unajumuisha aina mbili za kodi:

**a)** **Kodi za mazingira**- leseni, mirabaha, kodi za mauzo ya nje, n.k. ambazo zimeanzishwa ili kupandisha gharama za utumiaji wa maliasili katika uvuvi, uchimbaji wa madini, uvunaji wa misitu na uwindaji ili kupunguza utumiaji wa rasilimali hizo na kudumisha matumizi endelevu; na

**b)** **Tozo za huduma**- ambazo zimeanzishwa ili kupunguza gharama za huduma ya mazingira (kama vile kufanya tathmini ya athari kwa mazingira, au huduma za wasimamizi wa misitu), zinazojumuisha usimamizi au huduma za usafishaji zilizo muhimu kutokana na utumiaji binafsi wa maliasili.

Msisitizo ni kwamba kodi za mazingira hasa hupandisha gharama za mtumiaji ili kupunguza matumizi ya maliasili hadi kiwango endelevu.

Kwa sababu bidhaa za maliasili zenye thamani kubwa, kama vile mbao ngumu, zinahitajika sana duniani, hivyo kodi yake inaweza kuwa kubwa ili kupunguza uvunaji wa aina hii ya miti ya mbao.

Ni muhimu kuzingatia kwamba mapato yake yanaweza kuwa madhubuti, na hivyo kusababisha uwezekano mkubwa wa vitendo vya rushwa.

Uzoefu wa sehemu nyingine unaonyesha kwamba ni muhimu kuanzisha njia tofauti za ukusanyaji wa aina hizi mbili za mapato na ili kuepuka utegemezi mkubwa kwa tozo za huduma kama chanzo cha fedha cha mashirika yanayoshughulikia mazingira:-

a) Mamlaka za mapato za taifa, ingawaje ni vigumu kukomesha rushwa, zinaweza kuweka mbinu nzuri na zenye uwazi za ukusanyaji wa

kodi na uwezo wa kukusanya kwa ufanisi na bila uonevu.

b) Jukumu muhimu la mashirika ya mazingira ni kulinda mazingira na kusaidia shughuli za maendeleo endelevu. Pale ambapo chanzo chake cha fedha kinaanza kutegemea ada za leseni, kutakuwa na tabia ya kuweka ada na kuweka taratibu kwa namna ambayo itaongeza kipato kitakachokusanywa na si kuhakikisha matumizi ya maliasili katika kiwango endelevu.

c) Vilevile, mashirika yanayojishughulisha na mazingira yanaweza kusahau jukumu lao la msingi la kulinda mazingira na badala yake kuelemea kwenye mapato wayapatayo tu kupitia kodi hizo.

d) Pale ambapo vyanzo vya ndani vinatoa fedha kupitia njia bora za tozo za huduma na kodi za watumiaji, hizi zinakuwa za kiasi tu, na pia zilizotokana na kodi zisizo na uonevu: hiki si kitu cha kukitegemea katika kupata fedha za kutosha kugharamia mazingira.

Matatizo makubwa ya kiutawala yamehusishwa na mashirika yanayoshughulikia mazingira kupewa haki ya kuchukua sehemu, au kiasi fulani cha fedha wanayoikusanya kutokana na kodi za mazingira kama vile leseni za uvunaji wa misitu na kodi ya mauzo ya nje.

**Kisanduku 4.6**

**Mfano wa tatizo la utawala mbovu katika usimamizi wa maliasili**

Katika Tanzania, suala la taarifa ya misitu limevuta hisia za watu wengi. Taarifa ya Asasi ya Kimataifa inayosimamia usafirishaji wa viumbehai (Milledge na wenzake 2007) inakadiria kwamba 97% ya mapato hupotea, ambayo ni takribani dola za Marekani milioni 40 kila mwaka. Pia taarifa hiyo inaonyesha tofauti kubwa kati ya takwimu za bidhaa za misitu zilizouzwa nje zinazotolewa na mamlaka husika na zile za mamlaka ya China ambako bidhaa hizo huuzwa. Takwimu za biashara za mwaka 2004 zinaonyesha kwamba China imepokea mazao ya mbao toka Tanzania mara kumi zaidi ya vile inavyoonekana katika takwimu za Tanzania. Tofauti hii katika takwimu inaonyesha kwamba fedha zinakusanywa ila zinatumika vibaya au watoa takwimu hizo, labda wakiwa na mbinu na mashirika yanayojishughulisha na mazingira, wanakwepa kodi.

Baadhi ya taarifa zinazoweza kutumika katika kipindi cha mjadala na kuchangiamawazo.

**Kisanduku 4.7 Kiwango cha Matumizi ya Fedha za Umma kugharamia mazingira.**
**Utafiti unaonyesha kuwa sekta ya mazingira imekuwa inapangiwa matumizi kidogo ukilinganisha na jumla cha matumizi ya umma katika nchi zinazoendelea. Kwa mfano:.**

a) Katika nchi za Mali, Msumbiji na Tanzania chini ya 1% ya matumizi yote inapelekwa kwa mashirika makuu ya usimamizi wa mazingira.
b) Katika nchi ya Ghana, bajeti ya pamoja ya wizara za mazingira na sayansi na ardhi na misitu katika miaka ya 2003 – 2005 ilikuwa wastani wa 2% ya matumizi ya jumla ya serikali.
c) Katika nchi ya Mali, chini ya 1% ya matumizi yote yalipelekwa katika shughuli zote za utunzaji wa mazingira ikilinganishwa na asilimia 1.4 ya "utamaduni, vijana na michezo" na 1.9% ya "demokrasia na mambo ya nje".
d) Nchini Msumbiji, bajeti ya Mazingira ilikuwa 1.2% ikiwa chini kidogo ya bajeti iliyotengwa kwa Utamaduni, Dini na Burudani, ambayo ilikuwa 1.4 %.
e) Katika nchi hizi zote, watumishi wa serikali na wadau wengine, wote walikiri upungufu wa bajeti kwa sekta ya mazingira, na athari zake katika utendaji.

**Ulipaji wa huduma kwa mazingira (Payment for Ecosystem Services-PES)**

a) Hiki ni chanzo muhimu cha kuongeza fedha za kugharamia usimamizi wa mazingira na kinaweza kuwa na umuhimu mkubwa katika kuwanufaisha watu maskini.
b) Inapaswa kuzingatia kwamba ingawaje lengo kuu la PES ni kuhifadhi mazingira, inatokea uzingatifu wa mipaka na utekelezaji wa PES ili kuingiza faida za kupunguza umaskini na malengo ya mazingira katika miradi hiyo.

c) Hitaji kuu ni kwa pande zote, wanunuzi na wauzaji, kuboresha hali zaidi sasa wakiwa na PES kuliko walipokuwa hawana.

d) Inapaswa kusisitizwa kwamba watu maskini wanaweza kukabiliana na vikwazo maalum katika ushirikishwaji, ikiwemo uwezo mdogo wa kujadiliana bei kuliko wengine, wasiokuwa maskini.

e) Ni muhimu pia kusisitiza kwamba kama si watu maskini kuweka wazi haki zao za kisheria katika rasilimali zao, hawataweza kushirikishwa katika PES au hata kushiriki katika serikali ambayo ndiyo hufanya kazi ya kupatanisha.

f) Tafiti kadhaa zimebaini kwamba PES zinaweza kuwa ni sehemu muhimu ya kipato kwa kaya maskini. Kwa mfano, utafiti wa huko Nicaragua ulibaini kwamba wakulima wadogo wadogo wanaoshiriki katika vyama vya ushirika vinavyofanya biashara halali na yenye usawa ya kahawa, walikuwa na hali bora kuliko wale ambao walishiriki katika soko ambalo hubadilika badilika.

g) Pia inawezekana kwamba PES haikuandaliwa vizuri na haikutekelezwa vizuri na hivyo faida kwa watu maskini itakuwa kidogo kwani inaweza kuwa wanufaikaji wengi wa PES wakawa makabaila matajiri, kama ilivyo huko Costa Rica.

**Kisanduku 4.8 Tafsiri ya Matumizi ya Fedha za Umma**

**Kufasili matumizi ya umma katika mazingira na taarifa za matumizi ya umma katika mazingira, yaani PER**

Kipengele kimoja muhimu cha utekelezaji wa sera ni usimamizi wa rasilimali fedha. Hii ina maana kuhakikisha kwamba rasilimali iliyotengwa haibadiliki badiliki, na vipaumbele vya sera na rasilimali zinatumika kugharamia shughuli zinazochangia kufikiwa kwa ufanisi kwa malengo yaliyokusudiwa. Uelewa mzuri wa matumizi ya umma katika mazingira ni muhimu katika kutathmini ufanisi na ubora wa usimamizi wa mazingira.

Hata hivyo bado ufasili wa matumizi ya mazingira ni tata. Swanson na Lunde (2003) walieleza fasili mbalimbali na aina za ufasili huo (mifumo ya kuainisha matumizi) zinazotumika. Walibainisha, kwa

mfano, kwamba mashirika mengi yanayofanya utafiti wa matumizi ya umma katika mazingira au PER hayatumii fasili iliyo wazi kutokana na ukweli kwamba kuna maeneo mengi (na hasa vipengele vya kimazingira vya usimamizi wa maliasili) ambayo hakuna makubaliano juu ya nini hasa jukumu la sekta za umma katika maeneo hayo. Hivyo kumekuwa na tabia ya kuangalia makundi madogo madogo ambayo yamefasiliwa vizuri, ya matumizi ya fedha katika mazingira. Swanson na Lunde walipendekeza fasili pana na ya jumla ya matumizi ya umma katika mazingira: *"matumizi ya taasisi za umma kwa shughuli maalum zinazolenga moja kwa moja katika kulinda, kupunguza na kuondoa uchafuzi wa mazingira au aina nyingine yoyote ya uharibifu wa mazingira unaotokana na shughuli za binadamu, pia na shughuli za usimamizi wa maliasili ambazo hazijakusudiwa katika utafiti au uvunaji wa maliasili".*

Walipendekeza pia utumiaji wa mfumo wa uainishaji unaogusa mawanda mbalimbali ya matumizi katika mazingira, ambayo yanasaidia kubainisha uchangamano wa matumizi ya umma katika mazingira na utawala wa mazingira kwa ujumla wake:

- Mawanda ya mashirika: unatofautisha baina ya matumizi yaliyofanywa na mashirika halisi yanayojishughulisha na mazingira na wizara na mashirika mengine yenye uelekeo huo. Hii inasaidia kupima kiwango mwamko katika serikali.
- Mawanda ya kiuchumi: kuruhusu tofauti ya asili baina ya matumizi yanayojirudia rudia na ya mtaji, ambayo ni muhimu katika kuchanganua ufanisi wa kiufundi na umadhubuti wa matumizi.
- Mawanda ya kikazi: yanaelezea aina ya shughuli/kazi au huduma za kimazingira zilizotolewa na sekta ya umma – inaweza kujumuisha uandaaji wa sera, urekebishaji, shughuli za utekelezaji, kutoa huduma (kwa mfano, usimamizi wa taka), elimu ya mazingira, mafunzo, usambazaji wa taarifa n.k.
- Mawanda ya mazingira: yanaelemea uanishaji wa kimataifa wa matumizi ya umma yaani, CEPA na inatoa taarifa ya eneo mahsusi la mazingira ambalo kwalo matumizi yalifanywa ili kulilinda. Hii

inaweza kufaa zaidi katika ulinganishaji wa mawanda ya kikanda wa kimataifa: unatofautisha baina ya matumizi ya taifa na ya kikanda. Ni muhimu kutathmini mgawanyo wa rasilimali katika kanda mbalimbali.

- Mawanda ya ugharimiaji: yanaelezea vyanzo vya fedha, vinavyojumuisha vyanzo vya nje na vyanzo vilivyo nje ya bajeti.
- Mawanda ya programu/ masuala ya sera: yanaruhusu matumizi kupimwa dhidi ya sera.
- Vipaumbele (ambavyo vinahusishwa sana na programu).

***Chanzo:*** Swanson na Lunde (2003).

**<u>Maswali ya kupitia</u>**

**Ugharimiaji wa umma wa shughuli za mazingira:**

- Je, ipo fasili ifaayo ya "mazingira" inayoruhusu vipengele muhimu vya matumizi ya umma kugusiwa ipasavyo?
- Je, kipi ni kiwango cha jumla cha matumizi katika mazingira na ni kwa jinsi gani yanagawanywa katika mahitaji ya uwekezaji na bajeti?
- Je, ugawaji wa fedha unaonekana kufaa katika kushughulikia mahitaji makuu yanawiana na uwekezaji?
- Je, matumizi katika vipaumbele vilivyobainishwa havijabadilika?
- Vipi ni vyanzo vya fedha za matumizi ya umma ya kugharamia mazingira? Je, vyanzo hivi vinaathari yoyote katika matumizi endelevu?
- Je, ukusanyaji wa mapato ya ndani ndicho chanzo kikuu cha fedha za kugharamia mazingira? Je, kinatumika vizuri, kwa usawa na kwa uwazi?
- Ni kwa jinsi gani tunaweza kuongeza ushiriki wa sekta binafsi katika usimamizi wa mazingira?
- Nini kifanyike ili kutekeleza mageuzi ya mazingira?.

## Uzoefu wa matumzi ya Msaada wa Ujumla (GBS) katika bajeti

**Maswali ya tathmini**
**Matumizi ya Msaada wa Ujumla katika bajeti:**

- Ni kwa jinsi gani matumizi ya Msaada wa Ujumla katika bajeti yamesaidia sekta ya mazingira?
- Ni aina gani ya "viukilio vya mazingira" iliyojumuishwa katika mfumo wa tathmini ya Msaada wa Ujumla katika bajeti na ni kwa matokeo yapi?
- Ni kwa njia gani nyingine GBS imesaidia muktadha wa kitaasisi katika utekelezaji wa sera za sekta ya mazingira?
- Tunawezaje kuwa na uwekezaji toka nje wa moja kwa moja ulio na faida kwa watu maskini na kwa mazingira?
- Tunawezaje kuwa na mchango wa makubaliano ya mazingira ya kimataifa katika harakati za kupunguza umaskini?

Kitabu hiki kimetayarishwa na Ofisi ya Makamu wa Rais, Idara ya Mazingira ili kuwa mwongozo wa kufundishia kwa wadau wanaohamasisha umuhimu wa maendeleo endelevu katika juhudi na mikakati ya kupunguza umasikini.

Tunategemea kuwa walengwa hawa wakishaelewa kwa kina uhusiano uliopo kati ya umasikini na mazingira watakuwa ni mabalozi au wajumbe watakaosimamia ujumuishaji wa masuala ya mazingira kwenye sera, mipango, mikakati, programu na bajeti za maendeleo.

United Nations
TANZANIA
Delivering as One

**ISBN: 978-9987-9431-3-5**